

**MO SALAH KUKOSA MECHI MBILI AFCON**

UKURASA 21

**Makonda** akosoa DED kuchangisha wananchi kujenga zanahati

UKURASA 3



**'Shetani',** wenzake wafikishwa kortini tuhuma za mauaji

UKURASA 8

**MAISHA YALIVYO**

Fahamu kuhusu ndoa, taasisi isiyo na uzoefu,wenyeji

UKURASA 11


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Januari 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581562

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Dar 'yazama'

• **Mafuriko** yaua, yasomba hadi magari, manusura wasimulia... *Uk. 2*







Baadhi ya wakazi wa Tegeta kwa Ndevu, wilayani Kinondoni, wakiangalia nyumba zilizoharibiwa na maji baada ya Mto Tegeta kufurika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha Dar es Salaam jana na kusababisha maafa. Picha ndogo zikionesha sehemu ya barabara ya Kunduchi Mtongani ikiwa imekatika na ya Morogoro ikiwa imefurika maji eneo la Jangwani. **PICHA ZOTE: IMANI NATHANIEL**

## Waua mlinzi aliyekuwa zamu, wapora mali dukani


UKURASA 8

## Enzi mpya KKKT, Malasusa kuingizwa kazini rasmi leo

UKURASA 4



Askofu Dk. Alex Malasusa



Askofu Dk. Stephano Moshi



Askofu Dk. Fredrick Shoo

**MICHEZO** **MOROCCO: STARS TUTAINGIA KWA TAHADHARI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mvua ya alfajiri 'yaizamisha' Dar

**Na Waandishi Wetu**



Baadhi ya wakazi wa Tegeta kwa Ndevu, wakiangalia mabaki ya nyumba iliyobomolewa na maji, baada ya Mto Tegeta kufurika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha Dar es Salaam jana na kusababisha maafa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

MVUA kubwa iliyoambatana na upepo mkali iliyonyesha jana alfajiri mkoani Dar es Salaam, imeacha vilio kwa wananchi, baadhi wakipoteza wapendwa wao na wengine nyumba na mali kusombwa na maji.

Mbali na nyumba kubomolewa, kumeripotiwa vifo vya mifugo, magari kusombwa na maji na miti kuanguka.

Maeneo kadhaa jijini humo yakiwamo Tegeta na Jangwani yameathiriwa na mafuriko huku Daraja la Gwajima huko Tegeta Machinjioni, wilayani Kinondoni likibomolewa na kukata mawasiliano na wananchi kulalamikia kutozwa nauli kubwa baada ya kulazimika kutumia pikipiki. Baadhi ya madereva bodaboda walitoza nauli ya hadi Sh. 20,000.

**SIMULIZI WALIOJIOKOA**

Nicolas Palanjo, mkazi wa Tegeta Kwa Ndevu, wilayani Kinondoni, akizungumza na Nipashe Jumapili jana, alisimulia namna walivyokumbwa na mafuriko wakati wakiwa wamelala na watoto.

Alisema akiwa chumbani kwake, ghafla aliona maji yanaingia kwa kasi kubwa chumbani.

"Niliamka haraka nikaenda chumba cha watoto walikuwa watatu, akiwamo mtoto wa kaka yangu, Dorcas Palanjo (22), lakini kwa bahati mbaya Dorcas sikumkuta alikuwa tayari ameshasombwa na maji.

"Wenzake wawili (watoto wangu wa kuzaa) walijiokoa kwa kujishikiza kwenye kabati, tukafanikiwa kutoka nao salama," alisema.

Shuhuda wa tukio hilo, Magreth Mbando, mkazi wa Skaskca, alisema katika eneo hilo mtoto Ajra Juma (6), alisombwa na maji wakati akiwa ndani na mama yake.

"Mama aliamka baada ya mvua kubwa, kwa bahati mbaya mtoto akateleza na kusombwa na maji, bado waokoaji wanaendelea kuutafuta mwili wake, mama yake aliokolewa na wananchi," alisema.

Mjumbe wa Tegeta Machinjioni, Salum Mketo, alisema kuna familia nyingine imepoteza mama baada ya maji kujaa ndani ya nyumba yao.

"Baba wa familia hii alifanya jitihada za kumwokoa mke wake na mtoto wao wa miezi tisa, lakini kwa bahati mbaya mke wake aliteleza na kusombwa na maji," alisema.

Mmoja wa wananchi ambaye alikutwa na Nipashe akiokoa baadhi ya watu waliokuwa wamezingirwa na maji katika nyumba zao eneo la Tegeta Machinjioni, Jackson Ndeu, alisema waliamua kujitolea kuokoa maisha ya wenzao.

"Nikiwa nyumbani kuna jirani yangu akawa anasema kuna watu wanakufa huko, tukajikusanya vijana tulipofika eneo la tukio tukakuta maji yamejaa, moja ya nyumba maeneo hayo tulipochungulia dirishani tukasikia sauti za watoto wanalia, 'tunakufa... tunakufa'.

"Tukapanda juu ya bati tukabomoa dirisha tukafanikiwa kuokoa watoto wanne waliokuwa wakilia humo na tumemwokoa mtu mzima mmoja," alisema.

Pia alisema katika nyumba nyingine, waliporusha jiwe katika bati kama ishara ili kujua kama ndani mna mtu, ndipo walisikia mtu anapiga dirisha akiomba msaada na walifanikiwa kumtoa kwa kubomoa bati na kumtoa ingawa hakuwa katika hali nzuri kiafya.

Nipashe ikiwa eneo la tukio ilipata taarifa ya vifo vya watu wengine wawili, mwanamke na mwanaume wanaodaiwa kufariki dunia katika moja ya nyumba za kulala wageni maeneo ya Tegeta, kulikokumbwa na mafuriko hayo.

**RIPOTI YA TMA**

Taarifa iliyotolewa juzi na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilikuwa na maudhui ya tahadhari ya matarajio ya hali mbaya ya hewa kwa siku tano kuanzia Jumamosi hadi Jumanne.

Wakati kukiwa na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia jana, mkoani Dar es Salaam kwa mujibu wa taarifa ya TMA, angalizo la mvua kubwa lilitolewa katika maeneo machache ambayo ni mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe, Ruvuma na Kusini mwa Mkoa wa Morogoro.

Kwa siku ya Jumapili (leo), TMA ilitoa angalizo la mvua kubwa katika maeneo machache ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Morogoro, Lindi, Mtwara, Rukwa, Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe na Ruvuma pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

Taarifa hiyo pia ilitahadharisha kuwa kwa siku hizo mbili (Jumamosi na Jumapili) athari zinazoweza kujitokeza ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, pamoja na kuathirika kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi.

Taarifa nyingine ya TMA iliyotolewa jana ilikuwa na tahadhari ya matarajio ya hali mbaya ya hewa kwa siku tano kuanzia leo Jumapili, Mkoa wa Dar es Salaam ukiwa miongoni mwa maeneo yanayotarajiwa kukumbwa na hali hiyo.

TMA imehadharisha kuwa kwa siku mbili leo na kesho Jumatatu, kutakuwa na mvua kubwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Morogoro, Manyara, Arusha na Kilimanjaro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.

"Angalizo la mvua kubwa kwa siku ya leo Jumapili limetolewa katika baadhi ya mikoa ya Lindi, Mtwara, Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe na Ruvuma.

"Siku ya Jumatatu angalizo la mvua kubwa limetolewa katika maeneo machache ya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Morogoro, Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma.

"Angalizo la upepo mkali unaofikia kilomita 40 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofikia mita mbili limetolewa kwa baadhi ya ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi (mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia) pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)," TMA inahadharisha katika taarifa yake hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kwa siku ya Jumanne na Jumatano hakuna tahadhari yoyote iliyotolewa.

**TANAPA**

Katika hatua nyingine, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kupitia taarifa yake iliyotolewa jana na Ofisa Uhifadhi Mwandamizi, Kitengo cha Mawasiliano ya Shirika hilo, Catherine Mbena, lilitangaza kufunga kipande cha njia cha 'ARROW GRACIER'.

Catherine alisema kipande hicho hutumika na baadhi ya wageni kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia njia ya Machame, Umbwe, Lemosho na Londolosi.

Alisema kutokana na mvua ya mwaka huu inayoendelea kuwa kubwa na kusababisha maporomoko ya mawe, miamba ya barafu na utelezi, hivyo kuwa hatari kwa watumiaji wa njia hiyo.

"Ukaguzi uliofanywa na timu ya wataalamu ya Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA), ikishirikiana na wataalamu na taasisi ya NOLS (National Outdoor Leadership School) wenye uzoefu katika masuala ya usalama milimani, umeonesha kuwa hali imezidi kuwa mbaya.

"Maporomoko ya mawe, miamba ya barafu yameongezeka na kwamba kwa sasa si salama kwa watumiaji. TANAPA inasitisha matumizi ya kipande hicho cha njia.

"Na badala yake itumike njia ya kawaida ya kutokea Baranco kuelekea Karanga na barafu hadi kufika kileleni mpaka pale mvua inayoendelea kunyesha itakapokoma na kufanyika ukaguzi kujiridhisha kuwa njia hiyo ni salama kwa wapanda mlima na watoa huduma mlimani," alisema.

Catherine alisema kipande cha ARROW GRACIER kinaanzia karibu na Kituo cha Barnco katika eneo la 'LAVA TOWER' na kinapitia kwenye kasoko (crater) kuelekea kieleleni.

Alisema wageni kupendelea kupita eneo hilo kwa ajili ya kuona mandhari nzuri ya mlima na pia ni rahisi kufika kileleni.

**WAZIRI ALONGA**

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akizungumzia baa hilo, alisema tayari amemwelekeza Naibu Waziri wake, Godfrey Kasekenya kwenda Dar es Salaam na wakati huo alikuwa safarini kuungana na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na timu iliyoko huko.

Alisema lengo ni maeneo ambayo mawasiliano ya barabara yamekatika, hatua zichukuliwe kuyarejesha.

"Niendelee kuielekeza TANROADS kwa kushirikiana na TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) katika mitandao ya barabara kwa Dar es Salam na mikoa mingine kwa sababu mvua inaendelea kunyesha, kwa ushirikiano tulioelekezana na kushirikiana kule Hanang, Manyara, kuhakikisha tunajitahidi watanzania kupata mawasiliano ya barabara," alisema.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Tuntu Swebe**

## HABARI KITAIFA

UJENZI ZAHANATI

# Makonda amkosoa DED kwa kuchangisha fedha za ujenzi

**Na Beatrice Shayo,** PANGANI

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amemkosoa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, Isaya Mbenje, kuchangisha wananchi fedha kujenga Zahanati ya Kipumbwi.

Badala yake amemtaka kiongozi huyo atafute fedha ndani ya mwaka huu zahanati hiyo ikamilike, vinginevyo "afungashe virago vyake".

Makonda alielekeza hayo jana alipozungumza na wananchi wa wilaya hiyo, akisema ameshangazwa kuona zahanati hiyo inajengwa kwa michango ya wananchi badala ya halmashauri hiyo kuijenga.

Hata hivyo, Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya nchi inaelekeza kwamba wananchi wanaweza kushiriki shughuli za serikali yao.

Makonda alisema wananchi wanatembea umbali wa kilometa saba kupata huduma za afya, hali ambayo inahatarisha usalama wao wakiwamo wajamzito. Wakipatwa uchungu inakuwa ni changamoto.

"Mkurugenzi ninaomba uchukue kipazasauti, nimepita Kijiji cha Mwembeni wanalalamikia hawana kituo cha afya mwaka wa pili. Nikauliza kwanini, nikaambiwa kuna shida ilitokea lakini mbunge alitoa matofali zaidi ya 3,000 na mifuko ya saruji 100.

"Niambie kwanini kituo hicho cha afya hakifanyi kazi wananchi wanatembea kilometa saba? Ninaomba majibu," Makonda alisema.

Mkurugenzi huyo, katika majibu yake kwa Makonda, alisema zahanati hiyo ilijengwa kwa kiwango cha chini na kubomoka na tayari wananchi wameanza kujenga kwa michango aliyoitaja na wao katika bajeti ya mwaka huu wametenga kuwachangia ili waendelee na ujenzi.

"Lakini, tunaamini ifikapo mwishoni mwa mwaka huu tutakuwa tumechangia asilimia yetu na mwakani tunaweka sehemu ya pili ya umaliziaji wa ujenzi kwenye zahanati ya Kijiji cha Mwembeni," alijitetea.

Baada ya mkurugenzi huyo kutoa maelezo hayo, Makonda alihoji tena kama ifuatavyo:

**MAKONDA:** Mkurugenzi jukumu la kujenga zahanati ni la nani?

**MKURUGENZI:** Jukumu la kujenga zahanati ni la wananchi na serikali.

**MAKONDA:** Wananchi wana jukumu la kujenga zahanati?

**MKURUGENZI:** Ndio

**MAKONDA:** Hebu tueleze, ni kanuni ipi ama sheria gani inayomtaka mwananchi kujenga zahanati?

**MKURUGENZI:** Ni katika kushiriki kuleta maendeleo yao (Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya nchi).

Hata hivyo, Makonda hakuridhishwa na majibu hayo na kumtaka aeleze jukumu la msingi la kujenga zahanati ama kituo cha afya ni mpango wa nani na je, ni serikali au mwananchi.

Mkurugenzi huyo hakujibu chochote na kubaki kimya huku Makonda akiendelea kumtaka atoe majibu kwa wananchi.

"Kwahiyo, mkurugenzi hujui? Kwanini liwe ni jukumu la wananchi? Mwenyekiti upo wapi? Huu mwaka tafuteni pesa (fedha) kokote hiyo zahanati ndani ya huu mwaka ijengwe na ifunguliwe wananchi wapate huduma.

"Mkurugenzi usiposimamia hilo anza kupaki mizigo yako ustaafu kabla ya wakati maana umri wako ni mtu mzima hamwezi kuwaambia wananchi tutawachangia," alisema Makonda. Akizungumzia madai yaliyotolewa ya kunyanyasika wafanyakazi wa mkonge, Makonda alimpigia simu Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, kumtaka afike mkoani Tanga kutatua changamoto hiyo.

"Asili ya mkonge ni Pangani. Ni chanzo cha kipato kikubwa cha Taifa bahati mbaya Wanapangani wanateseka hasa wafanyakazi. Jumatatu ninataka (Katambi) ufanye kikao na wafanyakazi wote wa mkonge, tunataka maelezo Jumatatu," aliagiza.

Makonda pia alikabidhi pikipiki 14 kwa ajili ya makatibu kata wa CCM zenye thamani ya Sh. milioni 36.4 waende kufanya kazi kwa ajili ya chama na si kuzitumia kwa biashara.

"Tunapokea hizi pikipiki kwa furaha kubwa kuchochea shughuli za chama katika Wilaya ya Pangani. Ninaomba niwakabidhi makatibu kata wa CCM wa kata zote 14.

"Haya ni mapenzi ya Mbunge Juma Aweso kwa chama. Tumieni pikipiki kusikiliza kero za wananchi. Tumieni kufanya kazi ya Rais Samia. Tumieni pikipiki hizi kuongeza wanachama zifanye kazi ya chama," alisema.

Mbunge wa Pangani, Jumaa Aweso, ambaye ni Waziri wa Maji, alisema walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya barabara kwa kipindi cha muda mrefu na kwa sasa wamepatiwa mabilioni na serikali kwa ajili ya matengenezo.



Mwalimu wa mazingira wa Shule ya Msingi Mwanzo ya mjini Tabora, Furaha Komba akishiriki zoezi la kupanda mazao ya chakula katika viroba vilivyojazwa udongo maarufu kama kilimo mviringo, shuleni hapo juzi, ili kuendeleza ustawi wa lishe bora. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: NAM iendeleze ushirikiano katika ulinzi

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesisitiza Wakuu wa Nchi na Serikali Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) wahakikishe wanashiriki katika kila tukio la umoja huo pamoja na kuendeleza ushirikiano kwenye masuala ya ulinzi na usalama na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akihutubia katika Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za NAM ulioanza tarehe 15 - 20 Januari, 2024. Waziri Mkuu alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano huo.

"Tumezungumzia hali ya mabadiliko ya tabia nchi na namna tunavyopata athari kwenye maeneo yetu na umuhimu wa kuweka mkakati wa namna ya kudhibiti mabadiliko ya tabia ya nchi kwenye maeneo yetu," alisema.

Masuala mengine ambayo Majaliwa aliyawekea msisitizo katika mkutano huo ni pamoja na kutoa wito kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa kuangalia ajenda za NAM na kuona namna ya kushirikiana na NAM katika kuzitekeleza.

Mkutano huo wa siku mbili ulianza juzi katika Kituo cha Mikutano cha Ruwenzori, Speke Resort Kampala, Uganda. Katika mkutano huo Rais wa Uganda alikabidhiwa rasmi uenyekiti wa kundi hilo.

Mkutano wa NAM hufanyika kila baada ya miaka mitatu na mkutano wa mwisho, wa 18 ulifanyika jijini Baku, Azerbaljan mwezi Oktoba, 2019. Mkutano huo haukufanyika tangu mwaka 2019 kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19 lililoikumba dunia.

Mkutano huo unalenga kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya biashara, uwekezaji, kutokomeza umaskini, mabadiliko ya tabianchi, amani na usalama katika mipaka, sekta ya afya, mandeleo endelevu na uchumi wa kidijiti.

Umoja huo ulianzishwa wakati wa enzi za vita baridi ili kusaidia nchi wanachama wake kutoka mabara ya Asia, Afrika na Latin Amerika kuondokana na ukoloni ili kujitawala kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mapema juzi, Majaliwa alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Sri Lanka, Ranil Wickremesinghe. Pamoja na mambo mengine, walijadiliana kuhusu kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo mbili ikiwamo uwekezaji kwenye sekta ya madini na biashara.

"Bado taifa limeendelea na kaulimbiu yetu ya kuboresha diplomasia ya uchumi na tumewakaribisha Sri Lanka kuja kuwekeza kwenye sekta ya madini, viwanda na kilimo. Sri Lanka ni wanunuzi wazuri wa madini ya vito, kahawa, chai, korosho na mazao ya mboga," alisema.

Naye Ranil Wickremesinghe alisema nchi yake ipo tayari kuwekeza Tanzania na alimhakikishia Waziri Mkuu kwamba wako tayari kufungua ubalozi Tanzania ili kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na kurahisisha shughuli za uwekezaji na biashara.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba alisema miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa na viongozi hao ni pamoja na urahisi wa wananchi wa Sri Lanka kutembelea Tanzania na watanzania kutembelea Sri Lanka.


**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 153 of 2024**

**In the matter of the estate of the late NAFTALI ELINEEMA MSUYA of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for letter of administration by ALBART MSUYA and ELINEEMA NAFTAL MSUYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 7 day of February 2024
Dated at Dodoma this 14 day of January 2024

Resident Magistrate

Presented for filing this 14 day of January 2024

REGISTRY OFFICER

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 686 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE TALUMBA MAIKO TAMBULA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**
**NEEMA ALEX LIBONGI**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of 02/2024
DATED at MOROGORO this 19TH day of 01 2024

Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**YAH: MADAI YA TALAKA No. 1/2024**

**MDAI: NEEMA RICHARD KISSIMA**

**MDAIWA: MIRAJI SAID MSURI**

**KUITWA SHAURINI**

Ndugu MIRAJI SAID MSURI popote pale ulipo.
Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria tarehe 29/01/2024 bila kukosa.
Kama hukuhudhuria basi shauri hili litasikizwa upande mmoja na uamuzi utatolewa.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BUGENE
RESIDENT MAGISTRATE
PRIMARY COURT

# Enzi mpya KKKT, Malasusa kuingizwa kazini rasmi leo



Askofu Dk. Stephano Moshi.



Askofu Malasusa




Askofu Shoo

**Na Waandishi Wetu**

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), leo linaingia katika enzi mpya kutokana na kuingizwa rasmi kazini kwa Askofu Dk. Alex Malasusa, kuwa Mkuu Mpya.

Tukio hilo la kihistoria linafanyika katika Kanisa Kuu la Azania Front la KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Dar es Salaam na Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Mkuu wa KKKT anayemaliza muda wake, Askofu Dk. Fredrick Shoo, wa Dayosisi ya Kaskazini (Kilimanjaro), ataongoza tukio hilo akishirikiana na maaskofu wa kanisa hilo kutoka takriban Dayosisi 28 za kanisa hilo pamoja na maaskofu wa makanisa ya Kilutheri kutoka nje ya Tanzania na makanisa mengine rafiki.

Malasusa anarejea katika nafasi hiyo kwa mara ya pili baada ya kuongoza kanisa kwa miaka minane kuanzia mwaka 2007 hadi 2015. Anapokea kijiti kutoka kwa Askofu Dk. Shoo, aliyeongoza kanisa kuanzia mwaka 2016 hadi leo.

Wakuu wengine waliowahi kuongoza kanisa hilo ambalo sasa lina takriban miaka 61 tangu lilipoanzishwa mwaka 1963 ni Askofu Dk. Stephano Moshi wa Dayosisi ya Kaskazini (1963 - 1976), Askofu Dk. Sebastian Kilowa wa Kaskazini Mashariki (Tanga -1976 hadi 1992) na Askofu Dk. Samson Mushemba wa Kaskazini Magharibi (Bukoba) mwaka 1993 hadi 2007.

Mbali na Rais Samia, viongozi wengine mashuhuri waliothibitisha kushiriki ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma na viongozi mbalimbali wa serikali na vyama vya siasa wanatarajiwa kuhudhuria ibada itakayohitimishwa kwa kuingizwa kazini mkuu huyo.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya kanisa hilo, zilibainisha kuwa zaidi ya watu 1,500 wanatarajiwa kuhudhuria kuingizwa kazini kwa Askofu Dk. Malasusa na wakiwamo wageni kutoka zaidi ya nchi 20.

Katibu Mkuu wa KKKT, Mhandisi Robert Kitundu, akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii, alisema: "Watakuwapo watu mbalimbali na makanisa tofauti ambayo tuna uhusiano nayo kutoka Ujerumani, Marekani, Malawi, Kenya, Burundi, Msumbiji, Afrika Kusini na Ethiopia. '

Pia alisema KKKT imekuwa ikijihusisha na makanisa na vyama mbalimbali duniani ambavyo vimethibitisha kushuhudia tukio hilo kubwa.

"Hapa ndani tutakuwa na wageni tofauti ambao watatokea kwenye vyama mbalimbali kama Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Chama cha Biblia, makanisa ya kiprotestanti, Katoliki, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na viongozi wa serikali na vyama vya siasa," alisema na kuongeza kuwa washiriki wengine ni pamoja na wawakilishi wa mashirika na asasi za kiraia za kitaifa na kimataifa.

Pilikapilika za hafla hiyo zilipamba moto tangu juzi wakati Nipashe ilishuhudia eneo la Kanisa Kuu la Azania Front likipambwa huku wageni mbalimbali wakiwamo maaskofu wa KKKT na wale kutoka mataifa mengine ya nje, wakiwasili.

Askofu Dk. Malasusa alichaguliwa katika Mkutano Mkuu wa 21 wa KKKT uliofanyika Agosti 20 hadi 25, mwaka jana katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira Usa River, mkoani Arusha, baada ya mchuano mkali uliompa ushindi katika duru ya tatu.

Dk. Malasusa alichaguliwa baada ya kushinda kwa kura 167, sawa na asilimia 69.3 dhidi ya Askofu Dk. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi aliyepata kura 73, sawa na asilimia 30.3

**MALASUSA NI NANI?**

Askofu Dk. Malasusa alizaliwa Aprili 18, 1961 katika Kijiji cha Lukinga, Rungwe mkoani Mbeya. Wazazi wake ni Mchungaji Gehaz Malasusa (sasa marehemu) na Subilaga Mwakimi. Alibatizwa na Mchungaji Amon Mtwawa Julai 1961, katika Usharika wa Igonwe, Rungwe.

Alipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Rungwe (mwaka 1967-1969) na Bungo Morogoro mwaka (1970-1972) na sekondari kati ya mwaka 1973 na 1976 kidato cha kwanza hadi cha nne na baadaye mwaka 1978 hadi 1980 kidato cha tano na cha sita katika Shule ya Sekondari Kigurunyembe.

Mwaka 1981 hadi 1983 alijiunga na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa masomo ya stashahada ya usimamizi wa biashara wakati huo akiwa mfanyakazi wa uliokuwa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi (NPF sasa NSSF) katika Idara ya Ukaguzi wa Hesabu.

Kati ya 1988 na 1995 alikuwa mwanafunzi katika kilichokuwa Chuo cha Theolojia Makumira (sasa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira) akianza na ngazi ya cheti na baadaye Shahada ya Kwanza ya Theolojia (BD) na kuhitimu mwaka 1995.

Septemba 3, 1995 alibarikiwa kuwa mchungaji katika Usharika wa Maneromango, Kisarawe na aliyekuwa Askofu wa Kwanza wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Elinaza Sendoro.

Baada ya kubarikiwa kuwa mchungaji, Malasusa alipangwa kutumika katika Usharika wa Mburahati na baadaye Kisarawe ambako pia alikuwa Makamu Mkuu wa Seminari Ndogo ya Kisarawe. Pia alitumika katika sharika za Yombo na Msasani akiwa pia Mkuu wa Jimbo la Kinondoni kwa wakati huo, sasa Jimbo la Kaskazini.

Mwaka 1994 hadi 1996 alisoma kwa njia ya masafa katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki na mwaka 1996 - 1997 pia kwa njia hiyo hiyo katika Chuo cha Theolojia Vancouver, Canada, akichukua mafunzo ya muda mfupi kuhusu malezi ya vijana.

Pia alichukua masomo ya mwaka mmoja (1999-2000) yanayohusu Lugha ya Utamaduni wa Kifaransa, Paris nchini Ufaransa.

Desemba 21, 1996 Malasusa alifunga ndoa na Ericah Nkonoki katika Usharika wa Azania Front na wamejaliwa watoto watatu ambao ni Miriam, Michael na Mercy.

Mwaka 1994 hadi 2004, Dk. Malasusa aliitwa katika Umoja wa Kimisioni wa Kiinjili (UEM) Ujerumani na baada ya kufaulu usaili aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Vijana Kanda ya Afrika.

Wakati akiendelea na wajibu huo, Desemba, 2004 alichaguliwa kuwa Askofu wa pili wa DMP na baadaye kuchaguliwa kuwa Mkuu wa KKKT, katika uchaguzi uliofanyika Julai 18, 2017 katika Chuo Kikuu cha Makumira, Usa River, Arusha akichukua nafasi ya Askofu Dk. Samson Mushemba akiwa mwenye umri mdogo kuliko waliomtangulia na kuingizwa kazini Novemba 11, 2007 katika ibada iliyofanyika Azania Front.

Mbali na kuwa Mkuu wa KKKT, Askofu Malasusa pia aliwahi kuwa Makamu wa Rais wa Fungamano la makanisa ya Kilutheri Duniani (WLF) Kanda ya Afrika na Makamu wa Pili wa Mwenyekiti wa CCT.

Askofu Dk. Malasusa alipigiwa kura ya imani kwa mujibu wa Katiba ya Dayosisi kwenye Mkutano Mkuu wa 29 wa DMP uliofanyika Novemba 29, 2010 Bagamoyo mkoani Pwani na kuendelea na wadhifa huo hadi atakapostaafu au vinginevyo.

Kwa kutambua utumishi wake, Askofu Malasusa ametunukiwa shahada tatu za udaktari wa heshima kutoka Chuo cha Kilutheri cha Utatu Mtakatifu Amerika (Novemba 8, 2009), Chuo Kikuu cha Finlandia, Michigan nchini America (Mei 2, 2010) na Chuo Kikuu cha Helsinki, Finland (Mei 28, 2011).

**- Imeandikwa na Mwandishi Wetu (DAR) na Godfrey Mushi, ARUSHA**

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kushoto), akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iraq, Omer Berzinji pembezoni mwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi zisizofungamana na upande wowote (NAM), jijini Kampala,Uganda jana. Kwa mujibu wa Berzinji, Iraq ipo katika mkakati wa kufungua upya ubalozi wake hapa nchini hivi karibuni. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Waziri wa Ujenzi ashangaa ubovu miundombinu nchini

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashugwa, amesema ni aibu zama hizi za karne ya 21 Tanzania kuwa na barabara ambazo hazipitiki kipindi cha msimu wa mvua, hali ambayo inachangia baadhi ya shughuli za kiuchumi kusimama.

Bashungwa alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji maagizo aliyoyatoa kwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo kuhusu tatizo la maji kujaa juu ya barabara ya Dodoma-Morogoro na kukata mawasiliano katika kijiji cha Mtanana wilayani Kongwa.

Alisema ni aibu kwa taifa kama Tanzania ambalo limeingia kwenye uchumi wa kati wa chini, kuwa na miundombinu ya barabara ambazo hazipiti katika kipindi chote cha mwaka na kufanya shughuli za uzalishaji mali kusimama.

"Ni aibu kwa taifa letu ambalo limeingia kwenye uchumi wa kati wa chini na karne hii ya 21 kuwa na barabara ambayo ndiyo nyenzo muhimu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi kuwa hazipitiki eti tu kwa sababu ya mvua.

"Haiwezekani magari yanasubiri mvua zikatike ndiyo yaendelee na safari, watu wanasubiri hapa hadi nusu siku ndipo wapite, jambo hili halikubaliki," alisisitiza Bashungwa.

Kutokana na hali hiyo, waziri huyo alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi kutumia wataalamu wake kubaini tatizo la maji kujaa juu ya barabara hiyo na kulitafutia suluhu ya kudumu.

"Lakini katika suluhu ya muda mfupi mtakayofanya hapa mhakikishe haiharibu suluhu ya muda mrefu, siyo baadaye tena tuje hapa na hiki tulichokifanya kwa wakati huu kinakuwa hakina maana," alisema.

Aliagiza hadi ifikapo mwezi Desemba, mwaka huu, suluhu ya kudumu katika eneo hilo iwe imepatikana ili kuondoa tatizo la mawasiliano kukatika katika barabara hiyo muhimu kiuchumi.

"Barabara hii inatumika na mataifa mengine, sasa leo hii magari kushindwa kupita kutokana na maji kujaa kwenye eneo hili si sahihi kiuchumi," alisema.

Akikagua ujenzi wa barabara ya kilomita 33 kwa kiwango cha lami ya Kongwa- Mpwapwa, waziri huyo alisema serikali haitawavumilia makandarasi wababaishaji.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu miradi ya barabara ambayo imekuwa ikijengwa chini ya kiwango.

"Niwaagize Bodi ya Usajili Makandarasi pamoja na bodi ya wahandisi kuhakikisha mnachukua hatua kali kwa yeyote ambaye atafanya mambo kinyume cha maadili ya taaluma hiyo," aliagiza.

Alisema makandarasi ambao watashindwa kukidhi viwango, serikali itawaondoa kwenye orodha na kuwanyima zabuni za miradi mbalimbali.

Mbunge wa Mpwapwa, George Malima, aliishukuru serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, hali ambayo itasaidia kurahisisha mawasiliano hasa wakati wa masika.

"Mkoa wa Dodoma unazo wilaya saba, lakini hapa kwetu ndio wilaya pekee ambayo haikuwa imeunganishwa kwa lami, hivyo tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutuona wana Mpwapwa," alishukuru.

## Tanzania yashiriki mkutano wa NAM

**Na Halfani Chusi**

TAKRIBAN theluthi mbili ya nchi duniani zimekusanyika Uganda kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM), Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi hizo.

Katika mkutano huo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba.

Waziri huyo aliongoza ujumbe wa Tanzania katika mkutano wa siku mbili wa ngazi ya mawaziri uliokamilika juzi, akisisitiza Tanzania ni mwanachama hai wa jumuiya hizo.

Alisema Tanzania inashiriki kikamilifu katika ngazi zote za mikutano hiyo iliyoanza Januari 15, mwezi huu hadi kesho Jumatatu.

Pembezoni mwa mkutano huo, Waziri January alikutana na mawaziri wenzake kwa lengo la kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na nchi marafiki na kuweka mikakati ya kushirikiana kiuchumi.

"Nimeshakutana na Mawaziri saba wa Mambo ya Nje kutoka Kenya, Dk. Musalia Mudavadi, Somalia, Ali Omar, Ghana, Shirley Botchwey, Ethiopia, Demeke Mekonnen, DRC, Christophe Lutundula, Venezuela, Yván Gil Pinto na Bahamas, Alfred Seers.

"Nitaendelea kukutana na mawaziri wenzangu na agenda kubwa ni mikakati ya kuhakikisha kuwa Tanzania na nchi marafiki zinanufaika kwa kuweka mazingira rafiki ya biashara, uwekezaji na kuondoa changamoto zinazokwamisha jitihada za kukuza Uchumi," alisema Waziri January nje ya mkutano huo.

# Serikali yahimiza usimamizi wa utajiri wa rasilimali asili

**Na Enock Charles**

SERIKALI imehimiza jitihada za pamoja katika uangalizi na usimamizi wa utajiri asili uliopo nchini ili kuwa na uvunaji na matumizi endelevu katika kuleta tija na kuinua hali ya maisha kwa wananchi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, akifungua mafunzo kwa makatibu wakuu na wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara mbalimbali juzi jijini Dar es Salaam, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuweka mikakati ya uangalizi na usimamizi wa utajiri asili na maliasili za nchi.

Mafunzo hayo yana lengo la kuwajengea uelewa kuhusu sheria zinazoongoza usimamizi wa rasilimali hizo.

"Mafunzo haya yatasaidia kuweka mikakati ya pamoja katika uangalizi na usimamizi wa utajiri asili na maliasili za nchi zilete tija inayotakiwa kwa wananchi," alisema.

Waziri Pindi alisema mafunzo hayo yatawezesha uvunaji na matumizi ya maliasili hizo kuwa endelevu.

Alisema zipo baadhi ya nchi zilizoshindwa kusimamia vyema rasilimali za asili za nchi zao na kugeuka kuwa hasara kwao, hivyo kuwataka wakuu hao wa taasisi kushirikiana katika utendaji ili rasilimali hizo ziwanufaishe wananchi.

"Mmekutana leo (juzi), nina imani mtatoka na maazimio ya kuishauri serikali namna gani tunaweza kulinda rasilimali hizi asilia, kuwezesha utekelezaji na majadiliano ya mikataba ya uwekezaji katika utajiri asili.

"Kutokana na ukweli kwamba, suala la usimamizi wa mali asilia ni mtambuka linalohusu wizara, idara, taasisi, mashirika na mamlaka mbalimbali za serikali kwa kuzingatia hilo, wizara yangu iliona kuwa ili kwenda pamoja ni vyema kuandaa mafunzo haya," alisema. Katika mafunzo hayo, wakuu hao wa taasisi, pamoja na mambo mengine, walikuwa wanajadili sheria mbili zinazohusu mali asilia zilizotungwa mwaka 2017 ambazo ni Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili ya Mwaka 2017.

Pia Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba Inayohusu Rasilimali na Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017.

Kwa mujibu wa Waziri Pindi, lengo la kuzipitia sheria hizo ni kupata uelewa wa pamoja kuhusu sheria hizo na kupanga mikakati itakayowezesha katika usimamizi na uvunaji rasilimali hizo.

Alisema hiyo itasaidia kuunganisha wakuu hao wa taasisi za serikali katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali hizo.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tatizo la kuibuliwa kero ziara za viongozi liishe

**TAKRIBANI** kila zama ya uongozi, kumekuwa na matukio ya wananchi kuwashtaki viongozi wa maeneo yao kwa wakuu wa serikali au wa chama tawala kila wanapozuru mikoani ama kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo au uhai wa chama.

Matukio kama hayo yalikuwa mengi wakati wa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli. Baadhi ya wananchi katika mikutano ya viongozi, ikiwamo ile ya Rais mwenyewe, walikuwa wakitoa madukuduku yao kuhusu kero zao kutokutatuliwa. Mbali na kupewa nafasi kutoa malalamiko hayo, pia wamekuwa wakitumia mabango yanayoeleza madai mbalimbali kuhusu kutohudumiwa na viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, baadhi ya viongozi wa maeneo hayo, waliitwa na kutakiwa kutoa maelezo kuhusu madai hayo na miongoni mwao walichukuliwa hatua kwa kuondolewa katika nafasi na kupelekwa wizarani au kutenguliwa uteuzi wao.

Hata baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani, mambo hayo yameendelea huku katika baadhi ya mikoa akipokewa na mabango yenye ujumbe mbalimbali kuonyesha kuna kero katika sehemu hizo. Hali hiyo ilisababisha Rais Samia kueleza bayana kuwa hataki tena kuona mabango katika ziara zake na ikitokea hivyo, mkuu wa wilaya, mkoa, mkurugenzi wa halmashauri au watendaji wa sekta husika watakuwa hawana kazi.

Ni kweli kwa kiasi fulani baadhi ya wateule na watendaji waliodaiwa kutokutekeleza majukumu yao, waliondolewa.

Hiyo imekuwa ikijidhihirisha wakati wa uteuzi na utenguzi wa wakuu wa wilaya, mikoa na wakurugenzi unaofanyika mara kwa mara.

Mfano ni katika ziara aliyoifanya mwaka jana mkoani Mtwara kwa baaadhi ya wakuu wa wilaya, wakurugenzi na makatibu tawala kutenguliwa uteuzi wao.

Licha ya mambo hayo kufanyika kwa baadhi ya wateule kutenguliwa uteuzi wao kudhaniwa kungekuwapo na watu kujifunza, hali imekuwa tofauti, hivyo kuonekana sawa na sikio la kufa ambalo halisikii dawa.

Hilo limebainika tangu Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, alipoteuliwa kushika nafasi hiyo. Katika ziara yake ya kwanza Kanda ya Ziwa na inayoendelea sasa kuanzia Dar es Salaam. Katika ziara ya Kanda ya Ziwa, madudu mengi yalibainika katika sekta mbalimbali hali iliyosababisha baadhi ya viongozi wakiwamo mawaziri kuitwa na kueleza kwa nini kuna matatizo hayo na kuna mipango gani ya kutatua kero hizo.

Kujirudia kwa mambo kunaashiria kwamba kuna uwajibikaji mdogo kwa viongozi na watendaji waliopewa dhamana katika maeneo hayo.


Jambo la kujiuliza ni kwa nini matatizo hayo yanaibuliwa kila ziara za viongozi wa kitaifa zinapotokea? Je, viongozi hao wanatambua wajibu wao?

Kwa jumla, kujirudia kwa mambo hayo kunadhihirisha kwamba liko tatizo kubwa ndani ya serikali hasa ngazi za mikoa na wilaya ambako ndiko chimbuko na vuguvugu la maendeleo ya wananchi. Inashangaza kuona fedha nyingi zinapelekwa katika maeneo hayo lakini kero bado zinaendelea kuibuliwa.

Ni vyema tabia hii ya malalamiko ya wananchi kila viongozi wa kitaifa wanapofanya ziara mikoani, itafutiwe suluhu ya kudumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Rushwa ya ngono katika siasa imulikwe kwa jicho la tatu

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya vikwazo ambavyo huwa vinatajwa kukwamisha juhudi za wanawake kupata uongozi katika majukwaa ya siasa ni rushwa ya ngono, ambayo huwa inalalamikiwa na wadau wa siasa.

Rushwa hiyo inalalamikiwa kwa sababu inawarudisha nyuma na inawafanya wasifikie malengo ya kupata nafasi za uongozi, ili kushiriki katika ngazi za maamuzi wakiwa idadi sawa na wanaume.

Mwaka huu ambao ni wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa, ninadhani, ingekuwa ni vyema zikafanyika juhudi ambazo zitasaidia kumnyanyua mwanamke ili kuwe na uwiano kwa makundi hayo mawili.

Yanaweza kufanyika makongamano, warsha na semina kwa ajili ya kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi huo, lakini pia kuwafundisha mbinu mbalimbali za kuepuka rushwa hiyo.

Ninaamini wadau wa kutetea haki za wanawake wapo wengi, hivyo ungekuwa ni wakati wao kufanya kazi hiyo na ikiwezekana, rushwa ya iundiwe kitengo maalum katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ishughulikiwe yenyewe.

Kimsingi, rushwa ya ngono inadhalilisha utu wa mwanamke na kumvunjia heshima, na bahati mbaya huwa inaelezwa kuwa wapo baadhi ya wanawake hulazimika kutoa rushwa hiyo ili wapate uongozi. Ingawa muomba rushwa na mtoa rushwa kosa lao ni moja, ninadhani hili la rushwa ya ngono, kwa mazingira yake ninadhani yanahitaji kutengwa na rushwa nyingine katika kulishughulikia.

Ni vyema rushwa hiyo ingechukuliwa kama udhalilishaji wa utu wa mtu, vinginevyo, wanawake wanaweza kubaki na nafasi za viti maalum katika siasa, badala ya kusimama na kupambana na wanaume majukwaani.

> **Kimsingi, rushwa ya ngono inadhalilisha utu wa mwanamke na kumvunjia heshima, na bahati mbaya huwa inaelezwa kuwa wapo baadhi ya wanawake hulazimika kutoa rushwa hiyo ili wapate uongozi.**

Ninaeleza hivyo kwa sababu amayetoa, anawekewa mazingira magumu ya kupata uongozi ambayo hujikuta ameingia kwenye mtego bila kutarajia au asiingie na hivyo kukosa nafasi ya uongozi.

Binafsi ninaunga mkono juhudi zozote za kumkomboa mwanamke, kwani utoaji wa rushwa hiyo umekuwa ukiibua mijadala, huku wanawake wakilaumiwa, bila kufanya uchambuzi wa kina, ili kujua chanzo cha kuendelea kuwapo kwa rushwa hiyo.

Kama nilivyoeleza, rushwa hiyo inadhalilisha utu wa mtu, na sidhani kwamba kuna mwanamke ambaye kwa ridhaa yake anaweza kudhalilisha utu wake bali vikwazo anayowekewa vinaweza kuwa chanzo cha rushwa.

Hivyo, rushwa hiyo ingetanishwe na rushwa nyingine, kutokana na ukweli kwamba wanafanya hivyo bila ukubali wao, bali wanalazimishwa na kujikuta wamebanwa kwenye 'engo' na kulazimika kutoa.

Vilevile mfumo wa utoaji haki, ungetazamwe upya, kwani hata katika ofisi, wapo baadhi ya mabosi ambao wanaweza wasitamke wazi kutaka rushwa hiyo, lakini mazingira yanaweza kuonyesha kuwa anaitaka.

Mojawapo ya mazingira hayo ni kuzungushwa kutatuliwa tatizo, kuzuia jina wakati wa kuomba uongozi, kitendo kinachoweza kusababisha baadhi ya wanawake wakajikuta katika mtego wa kutoa rushwa.

Ni wazi kwamba mazingira hayo yanaumiza kusikia mwanamke amepata nafasi ya uongozi kwenye chama baada ya kutoa rushwa ya ngono au amejirahisisha mwenyewe ili apate nafasi anayotaka.

Rushwa hiyo ikiundiwa kitengo maalum cha kuichunguza kama wadau hao wanavyoshauri, wanaojipeleka au kujidhalilisha, lengo lao ni nini, badala ya kuwanyooshea videole na kumbe wanabanwa na mfumo.

## FIKRA MBADALA

# Wengi wape lakini wachache wasikilizwe



Pascal Mayalla

**Haki kuu ya pili ni ya kuchagua iliyotolewa na ibara ya Tano ya Katiba ya JMT. Haki hii ni kila raia wa Tanzania anapofikisha umri wa miaka 18, ana haki ya kuchagua kiongozi wake. Haki hii inatekelezwa kwa kila mtu kujiandikisha kupiga kura na haiwezi kuondolewa na mamlaka yoyote.**

MADA ya leo ni kuhusu Haki, Haki, Haki! Ya wengi wape lakini wachache pia wasikilizwe. Katiba ndiyo sheria mama inayotoa haki zote za watu wote wa Tanzania.

Hili ni ombi kwa jicho na sikio la Rais Samia Suluhu Hassan kuziangazia haki tatu kuu kwenye katiba yetu ambazo zimeporwa na serikali zilizotangulia.

Serikali, Bunge, Mahakama, hazina uwezo wala mamlaka ya kupora haki yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa katiba kwa sababu katiba iko juu na mihimili hiyo yote mitatu iko chini ya Katiba.

Mihimili miwili, Serikali na Bunge imepoka haki ya Mtanzania kuchagua na kuchaguliwa zilizotolewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ya mwaka 1977. Serikali na Bunge zilipata wapi uwezo na mamlaka ya kuzipora haki hizi? Mpaka ninapoandika hapa, haki hizi bado zimeporwa. Mtanzania hana haki ya kuchagua kiongozi anayemtaka kwa sababu haki ya kila Mtanzania kugombea imepokwa na kikundi kidogo cha watu wanaoitwa chama cha siasa.

Chama cha siasa ndicho kimepewa mamlaka ya kuamua nani agombee na si wagombea au wananchi, matokeo yake wananchi wanalazimishwa kuchagua viongozi walioletewa na vyama vya siasa kitu ambacho si sahihi kabisa, si haki na ni dhambi. Usikute ndiyo sababu karma kila siku inawatafuna viongozi wetu.

Rais Samia, analiishi jina lake la Suluhu kwa kauli na matendo kwa kuleta suluhu ya kweli ya mtanziko wa kisiasa unaolikabili taifa letu. Ameonyesha kwa kauli na matendo anataka maridhiano ya kweli ndiyo maana amekubali kubadili sheria mbalimbali.

Mabadiliko haya ni fursa ya kuzirejesha haki za msingi za Watanzania zilizoporwa. Kwa vile aliyezipora haki hizo si yeye bali kaingia na kukuta zimeishaporwa na sasa anafanya marekebisho tu ya sheria, lakini zile haki porwa za katiba haziguswi?

**HAKI KUU ZA MTANZANIA**

Haki ziko nyingi, lakini nitajikita kwenye haki tatu kuu za Mtanzania. Haki kuu ya kwanza ni ya uraia. Mtu yoyote akizaliwa ndani ya ardhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anakuwa raia wa Mtanzania kwa kuzaliwa. Haki hii ni haki ya kwanza ya msingi ambayo ni ya kuwa Mtanzania. Haki hii haiwezi kuondolewa na mamlaka yoyote, ila mtu anaweza kuipoteza endapo ataukana uraia wako.

Kwa mantiki hiyo, ile sheria yetu ya kuwa mtu akichukua uraia wa nchi nyingine yoyote, anaupoteza utanzania wake, ni batili na ni kinyume cha katiba. Hata hivyo, ubatili huu, haujabatilishwa kwasababu hakuna aliyefungua shauri mahakamani kuipinga.

Haki kuu ya pili ni ya kuchagua iliyotolewa na ibara ya Tano ya Katiba ya JMT. Haki hii ni kila raia wa Tanzania anapofikisha umri wa miaka 18, ana haki ya kuchagua kiongozi wake. Haki hii inatekelezwa kwa kila mtu kujiandikisha kupiga kura na haiwezi kuondolewa na mamlaka yoyote.

Kwa Tanzania, haki hii imefinyangwa finyangwa kwa baadhi ya watu kunyamaza kwa kufungwa gerezani, wagonjwa hospitalini na Watanzania walioko nje ya nchi.

Kutokana na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, uandikishaji unaotumia BVR hivyo kwa kutumia 'biometric data', kitambulisho cha taifa au passport ambavyo vyote vina 'biometric data', vinaweza kutumika kuwezesha Watanzania wote popote walipo kumchagua Rais wa Tanzania na wa Zanzibar.

Haki kuu ya tatu ni ya kuchaguliwa kupitia ibara ya 21 ya Katiba ya JMT.

Kwa mtu mwenye umri wa miaka 21, yuko huru kugombea nafasi yoyote ya uongozi kuanzia serikali za mitaa hadi serikali kuu. Haki hii ni ya msingi na haiwezi kuondolewa na mamlaka yoyote.

Hata hivyo, kwa Tanzania, haki hii ya kila Mtanzania ana haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi na kuchaguliwa imefutwa kwa kuchomekewa sharti la kudhaminiwa na chama cha siasa. Sharti hili ni batili.

**HITIMISHO**

Waungwana wanapotaka jambo lao kubwa, wakakaa pamoja kukubaliana na kukuta wamepewa kidogo ya kile walichotarajia, hawaziri, hawasusi wala kutaka kupeleka watu barabarani. Waungwana hupokea kidogo walichopata na kuendelea kuomba kikubwa.

Kwa vile matatizo makubwa ya siasa zetu yako kwenye Katiba, tulianza mfumo wa vyama vingi kwa katiba ya chama kimoja. Ili kuwatendea haki Watanzania, tunaendelea kumwomba kwa unyenyekevu Rais Samia aendelee kuliishi jina lake kwa kuleta suluhu ya kweli ya mtanziko wa siasa zetu.

Kwa mambo makubwa na mazuri anayoyafanya, Watanzania wengi wanamkubali. Lakini maoni ya wachache wanaotaka tufanye kwanza mabadiliko madogo ya katiba, pia yasikilizwe ili tufanye mabadiliko ya sheria ziwe za haki kwa wote. Wengi wape, wachache pia wasikilizwe.

**Mungu Mbariki Rais Samia**
**Mungu Ibariki Tanzania.**

**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kuingiza Jeshi mitaani kufanya usafi wapi na wapi?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

VIONGOZI! Viongozi! Viongozi! Nimekuiteni mara tatu! Nimekuiteni nikitaka mtwambie, hivi Jumatano ijayo ya Januari 24, mwaka huu, tunaandamana au tunafagia mitaa?

Viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mnawaambia wafuasi wenu kuwa siku hiyo ni maandamano ya kushinikiza kuondolewa miswada mibovu bungeni, kulalamikia gharama za maisha na kuheshimu maoni ya wananchi.

Ni maandamano yanayohanikizwa kufanyika katika Jiji la Dar es Salaam ambako wafuasi wa chama hicho tayari wameambiwa maeneo ya kukusanyika kupitia na kumalizia maandamano hayo, yanayosemekana kuwa ya amani.

Kwa kuwa yamepangwa kufanyika Dar es Salaam, Gavana wa Mkoa huo, Albert Chalamila, naye amewaambia wakazi wa jiji hilo, kuwa siku hiyo kutakuwa na usafi utakaofanywa na wanajeshi.

Hajaishia hapo akasema yeyote atakayekuwa mtaani akijifanya ni takataka, atazolewa na wanajeshi hao na kuishia dampo. Hapo sasa ndipo tunapochanganyikiwa na kujikuta njia panda.

Kwamba kama kuna maridhiano, ni vipi wakuu hawa wa pande hizi mbili wanashindwa kukaa pamoja na kukubaliana nini kianze kati ya usafi na maandamano!

Kama kweli kuna watu wamejiandaa kusafisha mitaa, inawezekana ni kwa ajili ya kuwezesha waandamanaji kupita bila kunukiwa na takataka, basi ingekubaliwa siku moja kabla usafi ufanyike na siku inayofuata maandamano yafanyike.

Au kama hilo haliwezekani, basi maandamano yafanyike siku moja kabla ya usafi, ili takataka zitakazokuwa zimetupwa mtaani na waandamanaji, zizolewe na wazoaji ili kuacha jiji likiwa safi.

Lakini unaweza kujiuliza, ni kwa nini basi wanajeshi watumike kufanya usafi wa Jiji wakati tuna kampuni zimesajiliwa kwa kazi hiyo, na zinalipwa na sisi wananchi tunaozalisha takataka hizo!

Mathalan kama ndivyo, kuwa sasa wanajeshi wetu wanataka kutumika kufanya usafi, sijui ni kwa sababu hatuna vita au nini? Mbona shuleni tulifundishwa kuwa kunapokuwa na amani hakuna vita, wanajeshi hutumika kuokoa raia kwenye majanga.

Juzikati tumemaliza kushuhudia wakiwa Hanang, Manyara wakiokoa na kuopoa waliokumbwa na maporomoko ya ardhi, likiwa ni moja ya majukumu yake ya kusaidia jamii. Lakini kama usafi wa mitaa ni sehemu ya kusaidia jamii, sawa.

Mwaka 2020 mwito wa maandamano kama haya, ulitolewa ukihamasishwa na mwanaharakati Mtanzania aishie Marekani, Mange Kimambi, akidai yangekuwa yasiyo na ukomo na kuitikisa serikali ya mkoa wa Dar es Salaam.

Mtikisiko huo ukamfikia Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Paul Makonda, akatangaza kuwa siku hiyo ya Novemba 2 ingekuwa ya usafi ukifanywa na wanajeshi. Hata hivyo hofu hiyo ilikuwa ya bure, hayakufanyika.

Chalamila anapita mlemle, akionya waandamanaji watarajiwa kuwa siku hiyo atakayekuwa mtaani kama takataka akimaanisha waandamanaji atajikuta amezolewa na kupelekwa dampo, maana yake lupango.

Mpaka sasa nashindwa kuelewa ni kwa nini jeshi linahusishwa na masuala haya ya kisiasa kwamba kiongozi mwenye dhamana ya kulinda usalama wa raia anapotaka kuzuia jambo hasi basi ahusishe jeshi kweli?

Siku zote masuala kama haya ya mikusanyiko, Jeshi la Polisi limekuwa likibeba dhamana kwa kuwa na jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao ikiwa ni pamoja na maandamano ambapo waandamanaji hupaswa kutoa taarifa za kuwapo mipango hiyo.

Jeshi la Polisi linapoona kuwapo ukakasi na viashiria vya uvunjifu wa amani na usalama, huwasiliana na watoa taarifa na kuwaeleza nini kimejiri na nini kifanyike na kuelewana, vinginevyo hutakiwa kutoa ulinzi kwa waandamanaji.

Kama Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais Samia Suluhu Hassan alishafungulia mikutano ya hadhara na maandamano ya amani, kuna sababu gani ya kusingizia usafi, ilhali hakuna viashiria vya uvunjifu wa amani?

Hivi kweli mwaka 1978 majeshi ya Uganda yalipovamia Tanzania na kufanya uharibifu, kama Chalamila angekuwa Rais na kubaini mapema kuwapo mipango ya uvamizi huo, angethubutu kuwaambia wanajeshi wakafanye usafi mkoani Ziwa Magharibi au wakabiliane na wavamizi?

Rais wakati huo, Mwalimu Julius Nyerere, alitoka hadharani na kusema: "sababu, nia na uwezo wa kuwapiga tunao" wala hakuzunguka mbuyu. Sasa kwa nini CHADEMA wasiachwe wakaandamana na mwishowe wakasikilizwa hoja zao?

Au kwa nini wasiambiwe ukweli tena kwa ushahidi, sababu za kuzuia maandamano yao badala ya kusingizia usafi wa mitaa, ambao haumo hata kwenye majukumu ya Jeshi? Mungu tusaidie Watanzania.

# Wafanyabiashara Pwani waomba maboresho soko

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAFANYABIASHARA katika Mtaa wa Kongowe, mjini Kibaha, mkoani Pwani, wameomba kuboreshewa mazingira ya soko ili wafanye shughuli zao katika maeneo salama tofauti na ilivyo sasa.

Kwa sasa wanafanya biashara zao katika eneo lisilo rasmi ambalo kipindi cha mvua bidhaa hunyeshewa na hivyo kuwa hatarini kuharibika na kupata hasara.

Katibu wa Wafanyabiashara wa Mtaa huo, Dotto Evarist, akizungumza na Nipashe jana, aliiomba halmashauri kuwaboreshea eneo hilo ili wafanye shughuli zao katika sehemu rafiki.

"Tunaomba serikali itusaidie kuboresha mazingira yetu ikiwa ni pamoja na kutusogezea huduma ya maji, umeme na choo na kutujengea vizimba vya biashara, tufanye shughuli zetu katika sehemu nzuri wakati wakitutafutia eneo mbadala.

"Pia tunaomba watakapotenga eneo litakalojengwa soko, lisiwe mbali na makazi ya watu, ili wateja watufikie kwa urahisi na bidhaa zetu ziuzike," aliwasilisha kilio chao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kongowe, Maimuna Jamhuri, alikiri kutokuwa na soko katika mtaa wake na kunasababisha wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika eneo ambalo si rasmi.

Pia alisema katika mtaa wake, barabara nyingi ni mbovu na hivyo kipindi cha mvua maji hutuama katika maeneo mengi, kero ambayo tayari ameiwasilisha kwa Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari.

Maimuna aliomba kituo cha polisi kufanya kazi saa 24 ili wananchi wapate huduma karibu tofauti na ilivyo sasa hufungwa saa 12 jioni na kunapohitajika msaada wa polisi, wanalazimika kusafiri kilomita 17 hadi Kituo cha Polisi Mji Mdogo.

Diwani wa Kongowe, Hamis Shomari, akizungumza kero ya soko alisema halmashauri imepanga kukarabati kwa kujenga paa na vizimba ili wananchi wafanye biashara katika hali nzuri.

Kuhusu changamoto ya barabara, Shomari alisema tayari amewasiliana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), hivyo baada ya mvua watafanya marekebisho sehemu korofi.

# 'Shetani' na wenzake wanne kizimbani tuhuma za mauaji

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MTINGWA Kilimanjaro (42), maarufu Shetani, mkazi wa Mbamba, mkoani Geita, pamoja na wenzake wanne wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Sengerema na kusomewa shtaka la mauaji katika kesi namba 1462/2024.

Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Sengerema, ASP Tito Mohe, akiwa na timu ya makachero, waliwakamata watuhumiwa hao kwa nyakati tofauti mkoani Geita na Shinyanga, wakiwa walikodaiwa mafichoni kwa mganga wa tiba asilia ambaye pia alikamatwa.

Akisoma mashtaka jana mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Tumsifu Barnabas, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mkaguzi wa Polisi Martha Chacha, aliwataja washtakiwa wengine kuwa ni: Majaliwa Damasi (22), mkazi wa Masumbwe, mkoani Geita na Mganga wa tiba asili, Emmanuel Damasi (34), mkazi wa Bulungwa, mkoani Shinyanga.

Wengine ni: Selina Mchele (49), mkazi kijiji cha Mwakilemwa, wilayani Sengerema pamoja na Maneno Mashauri (19), mkazi wa Kata ya Lwenge Sengerema, ambaye pia ni mwanafunzi wa kidato cha pili, katika Sekondari ya Lwenge wilayani humo.

Martha alidai washtakiwa hao kwa pamoja walitenda kosa hilo Oktoba 12, 2023, huko Bukokwa, wilayani Sengerema, kwa kuwaua Sophia Maduka (61) na mumewe Mathias Lusesa (71), wote wakazi wa Lwenge, wilayani humo, kinyume cha kifungu namba 196 na 197 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote na kurejeshwa rumande kutokana na mahakama hiyo kukosa mamlaka kisheria kusikiliza shauri hilo.

Hakimu Barnabas aliahirisha kesi hiyo hadi Februari Mosi, 2024 itakapokuja tena kwa ajili ya kutajwa.



Mwenyekiti wa kijiji cha Makundusi, wilayani Serengeti mkoani Mara, Joseph Museti (wa tatu kulia), akitoa maelezo kwa maofisa wa polisi mwishoni mwa wiki, kuhusu tukio la ofisi ya Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Kewambogo kuchomwa moto na watu wasiojulikana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waiba na kumuua Mlinzi akiwa kazini

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

WATU ambao hawakufahamika kwa haraka majina yao, wamevamia na kuvunja duka katika Mtaa wa Mwananchi, Manispaa ya Ilemela, mkoani hapa na kuiba vitu mbalimbali kisha kumuua mlinzi aliyekuwa lindoni.

Mlinzi huyo ameuawa kwa kushambuliwa kwa kutumia kitu chenye ncha kali katika sehemu mbalimbali za mwili wake.

Mmoja wa wamiliki wa duka hilo, Isack William, alisema alipofika dukani huko majira ya asubuhi, walikuta makufuri yamekatwa na taa zimenyofolewa na alipofungua mlango na kuingia ndani, alibaini bidhaa zimechukuliwa na mlinzi akiwa amelala huku kichwa chake kikivuja damu.

William alisema kuwa baada ya kushuhudia hilo, alimwita jirani yake ili amwangalie kama wanaweza kumpeleka hospitalini, lakini baada ya jirani huyo kufika walibaini alikuwa amefariki dunia, ndipo wakatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Kata ya Buzuruga, Catherine Thomas, alitaja hatua zinazoendelea kuchukuliwa za kuhamasisha na kusimamia suala la ulinzi na usalama katika mtaa huo ili kudhibiti uhalifu wa namna hiyo.

"Tayari tumeitisha kikao cha dharula ili tuone sasa ni kwa namna gani tunaanza na hili jambo, kwa maana tangu nimeingia katika uongozi ni tukio la kwanza kutokea," alisema Catherine.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Gideon Msuya, alisema tayari jeshi hilo limeanza uchunguzi ili kubaini wahusika wa uhalifu huo.

Msuya alitoa rai kwa wafanyabiashara wote mkoani humo kuajiri walinzi ambao wamepitia mafunzo na ambao wana uwezo wa kujihami ili kukabiliana na wahalifu wa namna hiyo.

# MAISHA

JANUARI 21, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14

## Kidevu bila upele

## MAISHA NI NYUMBA


Ukurasa 15

Mbao zinavyoendelea kutamba




## KATUNIKA


Ukurasa 16




## Mishikaki ya ndizi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | C | H | U | K | I |
| A | | | | S | | C |
| P | | D | A | I | | H |
| E | D | A | | K | A | A |
| N | | M | B | U | | C |
| D | | K | | | | H |
| O | T | A | N | A | | E |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

BAI, NAO, EDA, ZOA, OKOKA, USIKU, IGIZO, BANDO, UCHACHE, MATENDO


## AMSHA AKILI

WIKI HII TUNACHEMSHA AKILI KWA NAMBA. TAFUTA VIFUNGU VIFUATAVYO VYA NAMBA KATIKA JEDWARI HAPA CHINI. VIFUNGU HIVYO VIPO KUTOKA KUSHOTO KWENDA KULIA NA JUU KWENDA CHINI

**7391, 3645, 6034, 6658, 5116**


| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 0 | 2 | 1 | 7 | 0 | 5 | 2 | 8 | 3 | 2 | 8 | 3 |
| 0 | 1 | 8 | 7 | 6 | 2 | 4 | 6 | 6 | 4 | 9 | 6 | 6 |
| 7 | 7 | 1 | 4 | 7 | 9 | 9 | 0 | 0 | 5 | 5 | 7 | 4 |
| 3 | 5 | 1 | 1 | 7 | 0 | 8 | 2 | 0 | 8 | 0 | 7 | 5 |
| 9 | 9 | 7 | 8 | 4 | 2 | 8 | 6 | 0 | 4 | 9 | 5 | 3 |
| 1 | 3 | 9 | 3 | 9 | 0 | 0 | 6 | 6 | 8 | 2 | 6 | 0 |
| 1 | 7 | 2 | 7 | 7 | 6 | 5 | 8 | 1 | 3 | 0 | 4 | 0 |
| 7 | 6 | 8 | 7 | 9 | 6 | 1 | 0 | 6 | 9 | 8 | 4 | 9 |
| 9 | 3 | 0 | 6 | 6 | 5 | 1 | 6 | 5 | 2 | 4 | 7 | 7 |
| 1 | 4 | 1 | 8 | 8 | 6 | 6 | 1 | 7 | 9 | 3 | 7 | 6 |
| 0 | 3 | 9 | 3 | 5 | 5 | 3 | 7 | 8 | 5 | 7 | 7 | 0 |
| 5 | 1 | 2 | 5 | 2 | 7 | 7 | 9 | 0 | 6 | 9 | 1 | 3 |
| 6 | 6 | 5 | 8 | 2 | 3 | 3 | 9 | 2 | 6 | 9 | 1 | 4 |

## TOA TOFAUTI 5



# WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA

JOHN alikwenda sokoni kununua nyanya na mambo yalikuwa hivi.

John: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

Muuzaji: Kilo shilingi 1500

Kijana: Nimeagizwa unisagie tunataka kwenda kula na chipsi nyumbani

Muuzaji: Kijana usitanie kazi za watu

Swali
Chaza inapatikana sehemu gani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unajua ndoa ni taasisi isiyo na mzoefu wala mwenyeji?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee yanayojiri kwenye anga la Maisha Ndivyo Yalivyo. Tuko mwanzoni kabisa wa mwaka mpya 2024. Ni mwaka ambao watu wengi wana mipango na malengo mbalimbali kwa maendeleo yao na taifa kwa jumla.

Mwaka ulioisha wa 2023 wengi walikuwa na pilikapilika mbalimbali za kimaisha, ikiwamo ndoa nyingi kufungwa kwa wale waliokuwa na shauku ya kupata wenza wao. Wengi walifanikisha na matarajio yakiwa ni kutengeneza familia zilizo bora.

Hebu leo niongee kidogo na wanandoa hawa. Yapo mengi watu hujifunza ambayo hawajawahi kuyasikia popote, na wanaendelea kujifunza. Baadhi ni yafuatayo;-

Ndoa ni taasisi isiyokuwa na mzoefu au mwenyeji. Ni taasisi ambayo haina kufuzu na kwamba kama ukimweka Mungu pembeni hata kwa dakika moja, kila kitu kitaharibika.

Ni taasisi inayopingwa na shetani na mawakala zake kuliko taasisi nyingine yoyote maana anajua akishavuruga ndoa, familia jamii, nchi na hata ulimwengu utaathirika.

Msomaji wangu, ndoa ni mbio ndefu na siyo mbio fupi. Ni taasisi ambayo bila neema na huruma za Mungu kuwaatamia hamuwezi kupiga hatua yoyote.

Ni taasisi inayohitaji upendo wa matendo na siyo nadharia au maneno matupu! Ni taasisi pekee ambayo hakuna kuchekana wala kunyoosheana vidole.

Inahitaji kuombeana na kutiana moyo kwa namna ya kipekee maana hakuna mwanaume au mwanamke mwenye akili timamu anayeingia kwenye ndoa akiwa na wazo la kuja kuachana baada ya muda fulani.

Ndoa ni maisha halisi na wala siyo tamthilia au maigizo. Ndoa haiwezi kudumu kama hakuna uvumilivu wa dhati na kujituma kwa pande zote mbili.

Ni taasisi ambayo lazima ujifunze kusamehe hata kama wewe hutaombwa msamaha. Ni taasisi isiyohitaji ushabiki ila maombi tu. Hili ni jambo la muhimu sana!

Ni rahisi sana mtu aliye nje ya ndoa (hajaoa/hajaolewa), kukosoa, kutukana, kukejeli ndoa ya mtu mwingine. Na pengine kujifanya bingwa wa kushauri ndoa ya wengine. Lakini mtu huyu akiingia kwenye ndoa anakuwa mpole na mkimya kabisa.

Kila mtu anaingia kwenye ndoa kwa staili yake. Kila mtu anaoa au anaolewa na mtu wa aina yake tofauti na mwingine.

Kila mtu anaoa au olewa na mtu mwenye tabia tofauti, akili tofauti, msimamo tofauti, harufu tofauti na asili tofauti. Hivyo, bila uvumilivu na upendo wa kweli, unaweza kuchoka haraka sana.

Kwenye ndoa kuna majira ya kucheka na kufurahi. Kuna wakati ndoa inakuwa tamu kama asali, lakini kuna nyakati ndoa inakuwa chungu zaidi ya mwarobaini kiasi cha kutamani kurudi kwenu.

Lakini katika hali zote hizo kitakachoweza kuwasimamisha ni uvumilivu, kuchukuliana, kusameheana na kuachilia, kusitiriana na zaidi maombi ya neema.

Ndoa si kitu cha kujingamba, kujitapa na kujitutumua kuwa una ndoa nzuri kuliko wengine. Ndoa siyo kitu cha kujifanyia mashindano na jirani yako. Siyo sehemu ya majaribio, ni taasisi ya kuheshimiwa na kuombewa.

Mungu akikupa ndoa nzuri, mshukuru na ombea wengine ambao ndoa zao zinapitia tafrani mbalimbali. Wengi kutokana na kukosa uvumilivu, ndoa zao zimesambaratika. Zipo zilizoishia kuvunjika mahakamani, wengine wametengana kila mtu anaishi kivyake.

Lakini, kama nilivyotangulia kusema hakuna mtu anayeingia kwenye ndoa kwa matarajio ya kuachana muda mfupi ujao. Wanakuwa na malengo na maono katika kufanikisha safari yao ya ndoa.

> **“Kila mtu anaingia kwenye ndoa kwa staili yake. Kila mtu anaoa au anaolewa na mtu wa aina yake tofauti na mwingine.**

Msomaji wangu, kuingia katika ndoa kunahitaji umakini mkubwa sana. Mshirikishe kwanza Mungu atangulie safari yenu. Wengi walikurupuka wakaishia njiani ndoa zikiwa changa kabisa. Wakasahau kwamba wanapoandaa mipango yao ya maisha, adui naye yupo kazini akipanga mbinu za kuwaharibia.

Hata ndoa zilizodumu muda mrefu na kwa mafanikio makubwa, shetani haachi kuzivuruga. Hayo ni majaribu lakini kwa wanaomtumaini Mungu, huwasaidia kushinda yote.

Ndio maana katika moja ya maandiko yake anasema hakuna jaribu lisilo na mlango wa kutokea. Utatikiswa lakini usikate tamaa kwani njia ya kutokea ipo ukiwa mvumilivu.

Wengi wanakosa uvumilivu wanazikimbia ndoa zao hata kwa mambo madogo madogo. Lakini mambo yakizidi huku ukimtumaini Mungu, Yeye hufanya mlango wa kutokea, na kukuokoa.

***Wiki ijayo nitawapa mfano wa ndoa hizi. Je, una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Tuache fikra potofu, ‘red eyes’ si ushirikina

Siku kadhaa zilizopita, serikali ya Tanzania ilitangaza mlipuko wa ugonjwa wa ‘Red Eyes’ yaani macho mekundu.

Ni macho yaliyopata wekundu, yanayowasha na kuwa na viashiria vya damu (bloodshot).

Wataalam wa afya nchini wanasema wekundu huu hutokea pindi mishipa midogo ya damu chini ya uso wa jicho inapotanuka au kuvimba.

Kwamba mara nyingi, ni athari ya ukereketaji (irritation) au maambukizi (infection) ya kwenye jicho.

Macho mekundu yanaweza kuathiri jicho moja au yote mawili. Halafu si mambo yanayoibuka kimazingira mazingira kama baadhi ya watu wanaoamini ushirikina wanavyodhani.

Madaktari bingwa wa macho wanaeleza kwamba ni hali ambayo inaweza kutokea taratibu au kwa ghafla, kama vile kwa matatizo ya mzio au jeraha la jicho.

Nataka kusema nini? Nitajikita kuzungumzia hatari ninayoiona kuhusu baadhi ya Watanzania, hasa walioko pembezoni au vijijini, kupuuza tahadhari iliyotolewa na Wizara ya Afya namna ya kujikinga na maradhi haya.

Wako ndugu zetu huko pembezoni na hata mjini, ambao wanajikinga eti kwa kutumia dawa zisizo rasmi, wakiamini wameangaliwa vibaya na mahasimu wao kiuchumi, majirani na wasiopenda maendeleo yao.

Aisee, acha huo ujinga. Hakuna uhusiano wowote wa ugonjwa huu na ushirikina. Ukiona dalili nilizozitaja, nenda hospitalini daktari akusikilize, afanye uchunguzi na akuandikie dawa ili kuepuka madhara kwa kuwa dawa za macho ni tofauti na kwa matumizi tofauti.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Tiba katika Wizara ya Afya, Prof. Pascal Ruggajo, maambukizi ya ugonjwa huo kwenye ngozi ya juu ya gololi ya jicho yajulikanayo kitaalam kama viral ‘keratoconjunctivitis’. Ni maambukizi yanayosambaa kwa kasi kubwa.

Hakuna tiba maalum kwa ugonjwa huu na hata bila tiba, dalili huisha zenyewe ndani ya wiki mbili.

Taarifa zaidi zilizochapishwa katika tovuti ya Wizara ya Afya, zinaeleza kwamba kutokana na tabia ya ugonjwa huo kusambaa kwa kasi, maambukizi hayo huleta mlipuko unaosambaa kupitia kirusi kwa zaidi ya asilimia 80.

Kanzidata yao inaeleza kwamba kati ya Desemba 22 na Januari 11, mwaka huu, mkoa wa Dar es Salaam peke yake ulikuwa na wagonjwa waliojitokeza katika vituo vya kutolea huduma ya afya wapatao 869.

Iko hivi! katika maisha,poteza vyote ila usipoteze matumaini. Ukipoteza matumaini, umepoteza sababu ya kuishi kwa sababu, hasira ya mwanadamu haiwezi au kuathiri hitaji lake.

Ni muhimu kufanya uchunguzi wa afya yako, kwa kadiri utakavyoshauriwa na wataalam wa afya.


***•Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com. Simu ya mkononi: +255 715 545 490***

# HARUSI








Rangi ya pinki ni bora zaidi kwa maharusi kutokana na sifa yake ya kung'arisha. Pichani ni baadhi ya magauni ya mitindo mbalimbali ya rangi ya pinki unayoweza kuchagua katika sherehe za harusi.

# MITINDO








# MWANAMKE VIONJO

KUPENDEZA kwa mwanamke ni sanaa inayohitaji ubunifu wa hali ya juu ili kukupa mwonekano mpya kila siku.

Usitake watu wakuzoee kwa mtindo mmoja tu wa mavazi, lazima upende kubadilika badilika.

Unapokuwa na ubunifu wa kubadilika kimavazi na mapambo ni lazima watu watakuangalia kwa macho ya kushangaza kwa kutamani uwepo wako.



"Huyu mwanamke ni mrembo kila unapomuona anakuwa amependeza na anaonekana vizuri, karibu nguo zake zote zinampendeza"ni baadhi tu ya kauli za watu wakisikika wakisema mara anapopita.

Kupendeza ni vile unavyojipangia mwenyewe katika mavazi, aina gani ya nguo uvae kwa wakati gani na mahali gani.

Nataka nikwambie kwamba urembo ni sanaa, na rubani wa sanaa hiyo ni wewe mwenyewe anayehitaji kuwa mrembo, kinachotakiwa kuzingatiwa ni kufanya uamuzi sahihi katika chaguo lako katika nguo, mapambo ya kichwani na mwili.

Lakini kumbuka kwamba ni lazima uwe mjanja na mbunifu wa kubadili vionjo, usidumae na mitindo ile ile uliyozoea.

Ni vema ukajifunza kutafuta vionjo tofauti, naamini hakuna linaloshindikana, endapo utaweka bidii katika hitaji lako.

Kwa mfano, kama umezoea kuvaa nguo ndefu, siku moja moja badili na uvae nguo fupi kiasi, na usiwafanye watu wakuzoee kwa aina moja ya kionjo.

URAMBO

Na Mary Geofrey

# Kidevu bila upele inawezekana







TATIZO la kutoka vipele kwa wanaume wanaonyoa ndevu linaonekana la kawaida, lakini linaleta madhara kama halipatiwi tiba ya kudumu.

Vizuri watu wakaepukana na hali hiyo kwa kuchukua tahadhari, kama kutotumia wembe wa zamani na kutafuta tiba haraka kama likijitokeza tatizo hilo.

Sio wanaume wote wanapata tatizo la vipele na weusi kidevuni, ila kwa wale wanaokabiliwa nalo basi watambue inachangiwa na vitu vifuatavyo:

Kunyoa bila kulainisha ngozi, kupaka spiriti au 'aftershave' yenye 'alcohol' baada ya kunyoa.

Sababu nyingine ni kutopaka kitu chochote baada ya kunyoa na kutumia kiwembe kisicho na makali.

**Ufanye nini?**

Kulainisha ngozi kabla ya kunyoa ni jambo la muhimu kwa sababu sehemu ya juu ya ngozi ina chembe hai zilizokufa, na endapo ukilainisha ngozi kabla ya kunyoa itasaidia kuondoa chembe hai zilizokufa wakati wa kunyoa.

Pia itasaidia wembe kuteleza vizuri kwenye ngozi bila kusababisha michubuko.

Kutumia kilainishi cha 'aftershave' baada ya kunyoa ni suala la kuzingatiwa ili kupooza ngozi, kuipa unyevu nyevu na kufanya iwe nyororo.

Spiriti na aftershave zenye 'alcohol' zinafanya ngozi kuwa kavu, itasababisha miwasho na ukijikuna inatoka vipele.

Nyoa kwa kufuatisha muelekeo wa nywele zilivyoota ili kukusaidia ngozi isiumie zaidi. Pia hakikisha kiwembe unachotumia kunyolea ni kikali, kwani kikiwa butu utarudia mara nyingi na kuumiza ngozi.

Usitumie deodoranti yenye chumvi ya aluminium na alcohol kwani vipodozi hivyo vinachangia kufanya ngozi iwe kavu na kuwasha baada ya kunyoa ambayo itapelekea kupata weusi wa kwapa.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mishikaki ya ndizi

MAPISHI ya mishikaki ya ndizi, samaki wa kukaanga na maharage ya kuunga ni chakula kizuri kwa kuliwa na familia.

**Mahitaji**

Chukua ndizi, zimenye kisha zikatekate vipande vya duara, ndizi moja toa vipande sita na uweke kwenye mti wa mshikaki.

**Andaa mafuta ya kukaangia**

Maharage na tui zito la kwanza la nazi au unaweza kununua ya maji.

Samaki na viungo vyake vyote, unaweza kuweka kitunguu swaumu, limao na tangawizi.

**Jinsi ya kupika**

Chukua ndizi zako zikaange kwenye mafuta weka pembeni. Ukimaliza chukua samaki ambaye umeshamuungia viungo, mkaange naye umuweke pembeni.

Ukimaliza unga maharage yako vizuri yaweke nazi na usiyatie michuzi kabisa, chakula hiki kinapendeza kuliwa na mboga ya maharage ambayo ni kavu.

Ukimaliza andaa chakula chako mezani kitakuwa tayari kwa kuliwa.

Unaweza kushushia na juisi, chai na kinywaji kingine utakachopendelea kula.





MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba



KILA uchao tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna tofauti yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya leo.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yatakayofanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Na leo tunaangalia ubora uliopo sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni moja ya vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hasa pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo Msanifu Majengo, David Kashozi, anaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake.

Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.

"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anabainisha.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.





## DONDOO

Na Restuta James

WATAALAMU wanaeleza kuwa tangu matumizi ya mbao yalipogunduliwa, hazijawahi kushuka ubora na badala yake zinaendelea kushika kasi kwa kuboreshwa kila siku.

Inaelezwa kuwa katika karne ya ubunifu na uvumbuzi, mbao na hususani zile ngumu kama mkongo na mninga zimetumiwa kama marumaru (tiles), nakshi za dari, pambo la ukuta na 'holder' za taa.

Hata hivyo, ubunifu umekwenda mbali zaidi na kuja na mitindo mipya ya kipekee katika kuunganisha na umeme kama vile kuweka taa za juu, ukutani, nje na chini.

Kazi za kibunifu za msanii Ivan Cvitkovic, zilizochapishwa kwenye mtandao wa Pinterest zinaonesha pambo la vibao zaidi ya 20 vyenye taa likiwa kwenye ukuta na kuleta mwonekano wa kuvutia kwenye nyumba husika.

Kadhalika, mbunifu huyo ana aina nyingi za mbao kwenye taa za umeme na nyinginezo ambazo amezinakshi kwa kamba za katani.


Mbunifu mwingine aliyekuja na aina hiyo ya taa za ukutani ni Ziba Gailani, ambaye mbali ya mtindo wa vibao vidogo vidogo, ana aina ya vibao vipana vinavyowekwa kwenye ukuta mkubwa ndani ya nyumba au kwenye kibaraza kikubwa.

"Kwenye aina hii ya kutumia mbao na taa, unaweza kuamua taa ziwe katikati tu, juu, chini au kote, ni aina nzuri ya kupamba ukuta wako. Tatizo kubwa la mbao ni gharama," anasema fundi seremala Juma Suleiman.

Anasema hapa nchini, wapo wabunifu wa aina hiyo ya taa ambao wamebuni za mezani, 'stand' na muundo wa taa za umeme zinazofanana na chemli zilizokuwa zinatumia mafuta ya taa.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
HUU MKONO NIMEVUNJIKA 'GESTI' WAKATI NAREKEBISHA SHOTI YA UMEME 'CHUMBANI' 'NGAZI IKATELEZA!'
KWA HIYO YULE MKE WA MTU NDIO ALIKUWA 'TENESKO' MWENZAKO?
INAONEKANA MKEO HANA WIVU HATA AKIKUKUTA UMEKUMBATIWA KAMA HIVI JAMANI
ANDAA NAULI YANGU UNAKARIBIA KUSHUKA
MWANAUME ETI' UNARINGA KISA MTAANI UNAITWA HENDISAMU!
NA KWELI BABA WEWE UNGEITWA HENDISAMU UNA HAKI YA KUMFUNGA MTU JELA MAISHA!
USINIONE HIVI MIMI NIMEKULA CHUMVI NYINGI YAKUTOSHA!
KWA HIYO UNASUBIRI 'SAFURA?'
KONDA USINISOGELEE UTANIAMBUKIZA MIMACHO YAKO... ONA ILIVYKUWA MIYEKUNDU!
UTAIZIFUATA WAPI WAKATI TUMEKUTANA HUMU HUMU? WE MWEHU?
HAYA NIMEWASAMEHE ACHA DEREVA AKAWASHUSHE ATANIKUTA HAPA NAMSUBIRI
KWENDA ZAKO HUKO! SHIKA NAULI YAKO HAPA SIO MOMBASA
NINI?
SAWA BASI NAULI ZANGU NITAZIFUATA NIKISHAPONA NASHUKA!
KUTOKANA NA MIPANGO YAKO YA KUNIOA INACHUKUA MUDA MREFU...NIMEONA BORA NIOLEWE TU.
AFADHALI OLEWA NIOE!
UMENIPIGA BIA LAKINI SIJALEWA KABISAAA YAANI KAMA NIMEKUNYA MAJI SAFI
KWA HIYO HATA SUMU NILIYOKUWEKEA KWENYE BIA HAITAKUUA?
MVUA ZINAKUJA NA UPEPO HAKULALIKI NDANI NAOGOPA!
MBONA BADO UPO KITANDANI AU UNAJIONA UPO BARAZANI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...JIEPENDEKEZE UPATE SIFA UKWENI UKATAMBE KWENU

## HABARI KIMATAIFA

# Serikali ya Israel yagawanyika, wamtaka Netanyahu kujiuzulu

**TEL AVIV,** ISRAEL

SERIKALI ya Israel imeanza kugawanyika baada ya wajumbe wa Baraza la mawaziri la vita kumshutumu Waziri Mkuu, Benjamini Netanyahu kwa kutosema ukweli kuhusu malengo ya kijeshi kuhusu mapigano yanayoendelea Ukanda wa Gaza.

Mjumbe wa baraza hilo, Jenerali Gadi Eisenkol, amejitokeza na kueleza kwamba kinachosemwa na kiongozi huyo nje ya vikao hakina uhalisia na kwamba chombo hicho kimegawanyika katika misimamo ya kijeshi.

Hivi karibuni Netanyahu alikaririwa akieleza kukataa msukumo wa Marekani wa kutaka kuwepo kwa taifa huru la Palestina siku zijazo, na kusisitiza kuwa mashambulizi hayo yataendelea hadi ushindi kamili upatikane.

Hata hivyo, Eisenkot ambaye mtoto wake aliuawa alipokuwa akipigana Gaza, alisema wale wanaotetea suala la kushindwa kabisa kwa Hamas hawasemi ukweli kwa sababu kuna mgawanyiko ndani ya serikali na jeshi.

Jenerali huyo mstaafu alisema Netanyahu anawajibika kwa sehemu kubwa na kwa uwazi kwa kushindwa kwake kulinda nchi yake Oktoba 7, baada ya wanamgambo wa Hamas kufanikiwa kuingia ndani ya nchi hiyo na kuua raia na wengine kutekwa nyara.

Alisisitiza kwamba ni lazima kuitishwa uchaguzi mpya kwa kuwa hakuna imani na uongozi wa sasa wa Israeli.

Katika tukio hilo, Hamas iliwauwa takriban watu 1,300 na kuchukua mateka 240 katika shambulio lao la kushtukiza kusini mwa Israel.

Katika mvutano huo ndani ya baraza la mawaziri, inaripotiwa kwamba kuna kutoelewana kati ya waziri mkuu na Waziri wa Ulinzi, Yoav Gallanti.

Pia mvutano mwingine umeelezwa kujitokeza kati ya Israel na washirika wake wa karibu Marekani na nchi zingine za magharibi.

Baada ya Netanyahu kutoa maoni yake kuhusu utaifa wa Palestina, mshauri wa usalama wa taifa wa Ikulu ya Marekani, John Kirby alisema nchi yake na Israel zinaona mambo kwa njia tofauti.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani alisema kuwa hakuna njia ya kutatua changamoto za kiusalama ndani ya Israel kama hakuna taifa la Palestina.

Maofisa wanne wakuu wa vikosi vya usalama vya Iran wameuawa katika shambulizi linaloshukiwa kuwa la anga katika mji mkuu wa Syria.

Wakati huo huo, Jeshi la Ulinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu la Iran, limeilaumu Israel kwa kufanya shambulio ambalo limewaua washauri wake wanne wa kijeshi pamoja na wanajeshi kadhaa wa Syria.

Hata hivyo, Israel haijaeleza chochote kuhusu shambulio hilo.

Kwa miaka mingi imekuwa ikifanya mashambulizi katika maeneo yanayohusishwa na Iran ndani ya Syria.

Mashambulio hayo yameongezeka tangu kuanza kwa vita vya Israel na wanamgambo wa Hamas..

Shambulizi hilo lilifanyika jana katika kitongoji cha Mazzeh, kusini-magharibi mwa mji wa Damascus, eneo ambalo kuna uwanja wa ndege wa kijeshi, pamoja na makao makuu ya Umoja wa Mataifa,ubalozi na migahawa.

**BBC**



Wananchi wa DRC wakiwa katika uwanja wa Martyr jijini Kinshasa katika sherehe ya kuapishwa kwa Rais Felix Tshisekedi jana.
**PICHA : REUTERS**

## Maaskofu Senegal wapinga kubariki wapenzi jinsia moja

**DAKAR,** SENEGAL

MAASKOFU wa kanisa Katoliki nchini Senegal wamekataa kuwabariki wapenzi wa jinsia moja, kama kiongozi wao Papa Francis alivyoidhinisha hivi karibuni.

Katika kile kinachoonekana kuwa mabadiliko hayo ya kimafundisho yaliyohimizwa kiongozi huyo wa kanisa, yameonekana kutokubaliwa kwa viongozi wengi wa Kanisa Katoliki barani Afrika.

Katika tamko hilo ilielezwa kwamba uhalalishaji unaoendelea wa hila au uhalalishaji wa ushoga na upotovu mwingine wa kimaadili, maaskofu wa Senegal wanathibitisha kwa uwazi kwamba haitatolewa aina ya baraka za kilitrujia au za ziada kwa watu wawili wa jinsia moja.

"Ushoga unaelezewa kama ni ukengeukaji wa maadili na inachukuliwa katika Kanisa kama chukizo dhidi ya mapenzi ya Mungu," walisema maaskofu hao.

Katika kongamano la Mabaraza ya Maaskofu ya Afrika na Madagascar (SEEAM), ambalo linawakilisha Maaskofu wa Kikatoliki wa bara hilo, tayari lilitangaza kwamba baraka ya wapenzi wa jinsia moja haifai katika nchi za Afrika. Walisema baraka kama hiyo itakuwa inakinzana moja kwa moja na maadili ya kitamaduni ya Kiafrika.

# Rais Tshisekedi aapishwa kwa muhula wa pili

**KINSHASA,** DRC

Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi, ameapishwa jana kuongoza nchi hiyo kwa muhula wa pili wa miaka mitano.

Tshisekedi alitangazwa mshindi katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Desemba, hata hivyo matokeo yake yanapingwa na wagombea wa vyama vya upinzani.

Zoezi la kuapishwa kwake limefanyika katika uwanja wa michezo wa Martyrs jijini Kinshasa.

Rais Tshisekedi ataongoza taifa hilo kwa muhula mwingine wakati baadhi ya maeneo ya mashariki ya nchi hiyo yakiendelea kukabiliwa na ukosefu wa usalama, suala ambalo kiongozi huyo ameahidi kumaliza.

Viongozi kutoka mataifa kumi na nane wamehudhuria sherehe ya uapishaji, huku nchi nyingine zikiwakilishwa na viongozi waandamizi.

Tshisekedi aliingia madarakani kwa mara ya kwanza mnamo Januari 2019, baada ya kumshinda mgombea kutoka chama cha Joseph Kabila.

Rais Tshisekedi ni mtoto wa kiume wa mwanasiasa mkongwe wa upinzani marehemu Etienne Tshisekedi.

Awali kiongozi huyo alikuwa ameahidi kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa nchi hiyo ambayo inajivunia utajiri wa madini lakini raia wake zaidi ya milioni 100 ni maskini.

Pia katika kampeni zake aliahidi kukomesha mapigano yaliyodumu kwa zaidi ya miaka 25 mashariki mwa nchi hiyo.

Katika uchaguzi huo zaidi ya watu milioni 40 walijiandikisha kushiriki kupiga kura Desemba 20, kumchagua rais pamoja na wabunge wa kitaifa, mikoa na madiwani.

Rais Tshisekedi alitangazwa mshindi kwa kupata asilimia 73.47 ya kura.

Moise Katumbi, gavana wa zamani wa jimbo la Katanga, alibuka wa pili kwa kupata asilimia 18.08.

Martin Fayulu, ambaye pia anapinga matokeo hayo, alipata asilimia tano ya kura.

**RFI**

MAKALA

# NI MUHIMU SERIKALI KUSIKILIZA MAONI YA WANANCHI



Na Magabilo Masambu

**Siku hizi ukiingia kwenye mabasi, utaona pembeni ya kuta za basi kuna matangazo kwa abiria kwamba dereva akizidisha mwendo piga simu namba hizi. Kwa hiyo abiria wana haki ya msingi kabisa kupiga kelele kwenye basi wanapoona dereva amezidisha mwendo na kupiga kelele huko ni kulinda maisha yao binafsi na ya dereva pia kwa sababu gari likipata ajali yeyote anaweza kupoteza maisha.**

JAMHURI ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii."

Hii ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania yam waka 1977 ibara ya 8(a).

Duniani kuna aina nyingi za serikali. Ziko za kifalme, kijeshi na kadhalika.

Zile zinazoitwa serikali za watu, maana yake zinapata madaraka kutoka kwa watu, kama ilivyo serikali ya Tanzania.

Tafsiri yake ni kwamba zinawekwa na watu kupitia sanduku la kura ili zifanye shughuli za kustawisha na kuboresha maisha ya watu. Abraham Lincoln amewahi kusema kuhusu Demokrasia "Democracy is a government of the people by the people and for the people"

Ikiwa wenye serikali kwa maana ya wananchi wanapiga kelele juu ya jambo fulani, wajibu wa serikali ni kusikiliza kelele hizo na ikiwezekana kuzitatua na kwa kufanya hivyo, inajiwekea dhamana ya kuendelea kukubalika na kuchaguliwa kila wakati.

Kwa maana nyingine ni kwamba serikali wateja wake ni wananchi, yaani ni serikali ya watu kwa ajili ya watu.

Ikiwa kuna mtu fulani anamiliki mgahawa wa chakula akatokea mteja akanunua chakula kile, wakati anakula akagundua kwamba kwenye chakula kile kuna mawe mengi, akapiga kelele kwa mmiliki wa mgahawa maana yake mtu huyo anapenda aendelee kuwa mteja wa mgahawa ule, ndiyo maana anasema kuna mawe.

Jukumu la mwenye mgahawa si kumwambia kama ameona kuna mawe asile au akale kwingine.

Kama ni mwelewa kwanza, atamwomba radhi mteja wake ili asipoteze uteja huo, pili ataahidi kurekebisha ili siku nyingine mteja wake huyo arudi tena.

Siku hizi ukiingia kwenye mabasi, utaona pembeni ya kuta za basi kuna matangazo kwa abiria kwamba dereva akizidisha mwendo piga simu namba hizi.

Kwa hiyo abiria wana haki ya msingi kabisa kupiga kelele kwenye basi wanapoona dereva amezidisha mwendo na kupiga kelele huko ni kulinda maisha yao binafsi na ya dereva pia kwa sababu gari likipata ajali yeyote anaweza kupoteza maisha.

Ukimchapa mtoto haki alio nayo ni kulia. Inawezekana kilio chake kitakufanya unayemtandika umwonee huruma lakini ikiwa utamtandika mtoto halafu asilie wala kutoa chozi, maana yake mtandikaji anaweza kuchukulia kwamba mtoto yule ana kiburi cha kutosha, hivyo fimbo zitaongezeka japo imetokea mara nyingi. Mtu anatandika mtoto huku akimwambia nyamaza! Ukitaka anyamaze ni kuacha kipigo lakini huwezi kuendelea kumtandika huku ukitaka anyamaze. Huko ni kumnyika haki yake ya kulia.

Maana yangu ni kwamba ikiwa kijiji fulani hakuna maji wananchi wanalia, kazi ya serikali ya watu si kuwaambia kaeni kimya huku wakiwa hawana maji. Watakaa kimya kwa kuwekewa maji safi na salama.

Vivyo hivyo kwenye huduma zinginezo kama barabara, dawa hospitalini na shule, kilio cha wananchi si kuwanyamazisha bali kuwawekea huduma husika.

Tunatambua serikali haiwezi kutuliza vilio vya wananchi bila kutoa huduma zinazotakiwa na kutoa huduma hizo, inahitaji ushirikiano wa wananchi katika kutekeleza mipango kama inavyotamkwa na Katiba ibara ya 8(d) kwamba: "Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii."

Kushiriki huko lazima kuwe na makubaliano kati ya wananchi na serikali yao.

Kushiriki lazima kuendane na ushirikishwaji wa wananchi na serikali kwa maana ya viongozi wakubaliane kwenye mambo kadhaa ili kujiletea maendeleo ya pamoja.

Mfano, viongozi wanaweza kuwaeleza wananchi kwamba ili kutekeleza shughuli za maendeleo kama serikali, tumeona tupunguze matumizi ya serikali kwa kutotembelea magari ya bei kubwa na ninyi wananchi changieni hiki, ili tufanikishe maendeleo yetu maana ni yetu sote, wananchi wanaona naam kama viongozi wamefanya hivyo sisi tutafanya zaidi.

Sasa hivi ziko kelele za mabadiliko ya Katiba pamoja na sheria za uchaguzi. Wako waliotangaza maandamano.

Kama ambavyo yamekuwapo mazungumzo awali, ni busara pande zote kukubaliana kwa njia ya mazungumzo kwa sababu jambo hili ni la wananchi wote na serikali inapata madaraka yake kutoka kwa wananchi.

Wanaopiga kelele ni wananchi na kelele kazi yake huwa ni kuonyesha wapi lilipo tatizo. Tayari tumesikia baadhi ya viongozi wa serikali wakitoa vitisho.

Sasa tukijenga utamaduni wa kunyamazisha watu, hatutajua wapi tunapatia wapi tunakosea. Kusikiliza maoni ya wananchi na kwenda mezani ndiyo njia sahihi ya kutatua matatizo kama nchi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Unaenda ukweni unasikia wanakuteta*



Na Adam Fungamwango

SIKU moja jamaa alikwenda ukweni, ambako shemeji zake wanaishi. Huko ndiko alikoolea.

Alikuwa anakwenda kupeleka pesa kiasi cha shilingi elfu 20 za mchango wa arobaini ya msiba uliotokea upande wa mkewe. Alipofika kabla hajaingia ndani akasikia wanaongea. Walichokuwa wakikiongea ndiyo alichoka mwenyewe. Walikuwa wanamteta yeye na mkewe. Yaani jamaa wanamsema mpaka ndugu yao.

"Yaani hata shilingi elfu 20 inawapelekesha hadi leo hawajatoa. Watu wote wametoa kasoro dada yetu tu na mumewe. Ndiyo basi tena imetoka hiyo. Wakilipa mimi siyo Pili." Jamaa alisikia wakiteta.

"Uliona hata kwenye msiba, yaani tunaitana kutoa hela, watu wanachanga, wao wanajivutavuta tu." Mwingine akadakia.

"Na dada yule mwanaume amempata wapi? Yaani hakuona wanaume wengine akamchukua yule. Mwanaume hajielewi, hana hela, wenzake wamekuja na magari pale, yeye na mkewe kwa miguu, hawana hata aibu, afadhali basi wangekodi hata bodaboda, wamekuja wameongozana kama kumbikumbi." Bado walikuwa wanaendelea kuwateta.

"Ndiyo maana kwenye msiba au tukikutana yeye ndiyo anatumwatumwa kwa sababu hana pesa, kapuku wa kutupwa, wenzake wamekuja na magari, utawatuma?"

Jamaa aliyasikia mwenyewe kwa masikio yake. Awali alidokezwa kuwa shemeji zake pamoja na kwamba wanaonekana wanampenda wanapokutana, lakini wanamchekea jino pembe tu.

Alichofanya ni kuingia ndani ghafla bila kupiga hodi. Shemeji zake ambao wote watatu walikuwa wa kike, walipomuona walishtuka na kuanza kujibiraguza.

Halitaka kuwaficha, akawaambia kuwa walichokuwa wanaongea amekisikia. Ila hatojibu kitu na alichofuata pale ni kutoa pesa ya mchango arobaini ya msiba.

Pamoja na kwamba wao walisema kuwa yeye na mkewe hawatolipa, wamefanya hivyo. Akaiweka mezani, hakuaga akaondoka. Wakabaki wanaangaliana kila mmoja akishindwa hata kumlaumu mwenzake.

Mambo haya yapo sana kwenye jamii yetu.

Wapo ndugu ambao wanasema wenzao kwa sababu tu wao wana uwezo na mwenzao hana.

Wanashindwa kutambua kuwa hata kama mkizaliwa kumi kwenye familia, siyo kwamba kila mmoja atakuwa na hali sawa na mwenzake.

Watatofautiana vipato, uwezo, vipaji, elimu na vitu nyingine vinavyofanana na hivyo.

Hata kama ni watoto wa kike watapoolewa, wote hawawezi kuolewa na wanaume wanaofanana uwezo na kila kitu.

Sasa hii isiwe sababu ya wengine kuwadharau na kuwasengenya wenzao. Mungu anampa kila binadamu na riziki yake.

Akimpa leo huyu kesho atampa mwingine.

Ndugu unayemcheka na kumdharau kesho ndiye atakayeikomboa familia hiyo hiyo wakati wengine wameshakula pesa zao, wamepata maraha sana na sasa wako hoi bin taaban.

Katika hili kikubwa ni kuwa pamoja na kusaidiana. Kwa nini wale wenye uwezo wasiwasaidie ndugu zao ambao hawana uwezo mkubwa badala ya kuwasengenya?

Hili nililolihadithia hapa lipo katika wimbo uliotwao 'Uteti', ambao ulipigwa mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1980 na bendi ya UDA, iliyokuwa ikimilikiwa na Shirika la Usafiri Dar es Salaam (sasa UDAT).

Ulitungwa na mwanamuziki mwimbaji chipukizi wakati huo, lakini akaondokea kuwa staa mkubwa nchini, akipigia bendi mbalimbali kama Mwenge Jazz, DDC Mlimani Park Orchestra, Vijana Jazz Band. Huyu si mwingine bali ni Benovilla Antony.

Akiwa na bendi ya UDA Jazz ambayo ni kama ilimtambulisha kwenye ulimwengu wa muziki, alitunga kibao hicho kilichojichukua umaarufu mkubwa na kumfanya asikae sana katika bendi hiyo, akanyakuliwa na Mwenge Jazz, bendi inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Hebu pitia mashairi ya wimbo huu uone watu wenye tabia hiyo ambayo haikubaliki kwenye jamii.

"Siku moja nilipokuwa eee, natembelea kwa shemeji zangu, kitu kilichonishangaza sana njiani, ni kujiakwa kila mara. Kabla ya kuingia ndani nilisikia vicheko dirishani, nilisita kuingia ili nisikie kile kinachowachekesha. Kumbe ulikuwa uteti, kuhusu sisi mimi na ndugu yao, nilipoingia ghafla waliona haya, sikukaa nikaondoka.

"Muone haya, muone haya, muone haya, muone haya, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe. Nicheke na nani, ooo na nani, niongee na nani, ooo na nani, iwapo ndugu zangu wenyewe mnanisengenya yoyoyoyo.

"Muone haya, muone haya, muone haya, muone haya, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe. Mliyoyasema yote nimeyasikia, lakini mjue yote hayo mmetunga, hamkuanza leo kutusengenya wana wa wenzenu yoyoyo.

"Muone haya, muone haya, muone haya, muone haya, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe, mara nyingi nimeambiwa mwaniteta, na sasa nimesikia mimi mwenyewe."

Watetaji wamefumwa laivu, ni aibu kubwa, haikupaswa kuwa hivyo, huwezi kumteta ndugu yako mwenyewe badala ya kumsaidia.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu - 7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

KWANZA kabisa ukumbini akakutana na michanga ambayo iligandamana na majimaji, ikionyesha kabisa kuwa ni kama hakukufanyika usafi wowote, au mpiga deki alimwaga michanga baada ya kufanya hivyo.

Akafungua mlango wa geti la nje. Alichokutana nacho kilimshangaza. Uwanja ulikuwa na majani ya mti mkubwa uliokuwa kando ya nyumba hiyo.

Alikutana na majani mengi makavu ambayo yalikuwa yamesambaa uwanja mzima kama vile hakukufagiliwa.

Kilichomshangaza zaidi ni kwamba si jambo la kawaida kwa muda wa alfajiri ambao alikuwa amefagia, majani mengi makavu yawe yameanguka tena kwa muda ule mfupi tu.

Akaenda moja kwa moja hadi bafuni na kumalizia chooni. Kote alikuta kuchafu kama vile hakukufanyiwa usafi wowote.

Ilimshangaza, lakini akili yake ilikuwa timamu. Hakuwa kwenye ndoto alipoamka kufanya usafi.

Akatoka tena nje na kwenda jalalani eneo ambalo alitupa majani makavu baada ya kuyafagia.

Alichofikiria kilikuwa sahihi. Wifi yake alikuwa nyuma ya yote hayo. Ni yeye ndiye aliyeacha wifi yake amalize usafi wote na kuanza kuchafua kwa makusudi.

Alianza bafuni na chooni. Akachota michanga na kumwagia ukumbini. Halafu akaenda kule alikomwaga majani makavu akakarudisha tena uwanjani na kuyasambaza ili ionekane hakujafagiliwa kabla ya kwenda kumuasha mke wa kaka yake.

Sauda alijawa na hasira isiyomithilika. Kuna sauti ilimjia ikimtaka kwenda kumpiga wifi yake, lakini ikajitokeza nyingine ikamkataza. Akatulia.

Halafu akawa amejiandaa kwenda kumkoromea na kumpa vipande vyake kuwa yeye ndiye aliyechafua. Hilo nalo aliliahirisha baadaye.

Akaona cha kufanya ni kurudia tu kufanya usafi ambalo ndilo lengo la wifi yake.

Akajua lengo ni kumsumbua arudie tena kusafisha, au aache ionekana ni mvivu, hafanyi usafi.

Akarudia kupiga deki, akaenda kufanya usafi chooni na baadaye akaenda kufagia uwanjani, tayari kweupe jua linawaka.

Wifi yake Havijawa alikuwa chumbani kwake. Mara kwa mara alikuwa




**"Usimuogope Sauda, sisemi kama umpige, au mpigane, lakini usiwe mnyonge, akikubwatukia na yeye mbwatukie, atakuogopa. Usimuendeleze. Hutoona raha ya ndoa na ipo siku utaamua tu kufungasha virago urudi nyumbani."**

anatoka na wakati mwingine kumchungulia Sauda akirudia kufanya usafi.

Akafurahi na kucheka kimoyomoyo kuwa alichokuwa anakitaka kimefanikiwa.

**********************************

"Sauda shoga yangu mbona umekonda hivi? Yaani ndoa haijakupenda kabisa! Wenzako wakiolewa wananawiri, wanakuwa wameachana na shida za nyumbani kwao kupangiwa muda wa kulala na aina ya chakula, lakini kwako unalala unapojisikia, unakula unachokitaka, leo imekuwaje Sauda?

Yaani siyo Sauda yule ninayekufahamu wakati hujaolewa, ulikuwa mrembo mwenye furaha na tabasamu mdomoni, nini kilichokuta mama?"

Maneno yale yalionekana kumchoma moyo Sauda akajikuta tu ghafla machozi yakimtiririka, na baadaye akaanza kulia kwa sauti.

Ilibidi rafiki yake aanze kumbembeleza. Alikuwa amekwenda kumtembelea mmoja wa marafiki zake ambaye alikuwa anakaa nao kibarazani kipindi kile kabla hajaolewa.

Ndiyo sehemu ambayo Kassim alikuwa akipita mara kwa mara na kuvutiwa naye.

Baada ya kumbembeleza kwa zaidi ya dakika 10, Paulina akamuuliza tena shoga yake.

"Vipi Sauda, kwani wewe huni?"

"Nakula Paulina."

"Tatizo nini, mateso shoga yangu? Au umeikuta ndoa ndoana?"

"Wala siyo hivyo shoga yangu. Na wala tatizo siyo mume wangu!"

"Kumbe nini Sauda, maana siyo Sauda wewe ninayekujua, umeisha umebaki mabega juu kama umetundikwa kwenye mti, niambie mimi rafiki yako, kama usiponiambia mimi utamwambia nani?"

"Rafiki yangu, haya yote unayoyaona tatizo ni wifi yangu!"

"Wifi yako?"

"Ndiyo Paulina!"

"Huyu aliyeachika Keko akarudi kwao?"

"Ndiyo."

"Sauda weee shoga yangu, yaani wifi ndiye anayekufanya unyorodoke hivyo?"

Akatumia muda huo huo kumsimulia maswahibu yote yanayomkuta, ikiwemo la juzi tu kufanya usafi, lakini wifi yaka akapita tena kuchafua na kwenda kumwita arudie tena.

"Usimuogope Sauda, sisemi kama umpige, au mpigane, lakini usiwe mnyonge, akikubwatukia na yeye mbwatukie, atakuogopa. Usimuendeleze. Hutoona raha ya ndoa na ipo siku utaamua tu kufungasha virago urudi nyumbani."

"Sasa unanishauri vipi shoga yangu Paulina?"

"Pigania ndoa yako! Ndoa inakufa kwa nyinyi wenyewe wapenzi kugombana na siyo kwa sababu ya mtu mwingine ya pembeni, huo ni uzembe Sauda."

"Basi nimekuelewa."

"Ndiyo, inawezekana wifi yako anakufanyia visa ili ukasirike uondoke. Inawezekana kuna msichana shoga yake anataka kumtengenezea nafasi, usichoke, ndoa yako bado changa sana rafiki yangu."

"Nimekusikia Paulina."

"Na hivi bado, yaani atakutengenezea visa ili mradi umchukie mumeo uondoke, usiruhusu hicho kitu. Usimchukie mumeo kwa sababu ya kikaragosi kimoja."

"Lo! Nashukuru shoga yangu kwa kunitia moyo, naahidi nitafanya kama ulivyoniambia."

"Haiwezekani ndoa hii ivunjike kirahisi hivi wakati mapenzi yalipoanza kuchipuka tulianza kushuhudia wenyewe jinsi Kassim alipokuwa anapita hapa mtaani kwa dada yako, kila akipita anakukuta uko na mdoli wako, atakaa upe jina, ukamwambia atoe yeye, akatoa jina la Matokeo na mpaka matokeo yake ikawa ndoa, leo ivunjike!

Mimi niliyeanza kuwaita baba na mama Matokeo siwezi kuwa radhi mpaka mtoto azaliwe nimwite Matokeo kama mlivyouita ule mdoli wenu ndiyo nitaridhika."

Sauda aliangua kicheko na kusahau kama muda mfupi tu uliopita alikuwa akilia.

Akakumbuka jinsi Kassim alipokuwa akipita eneo lile, ambapo baada ya kuwazoa akaanza kuwatania, huku yeye ndiye akitaniwa zaidi kutokana na kila alipokuwa akipita alikuwa amepakatia mdoli.

Alikumbuka mbali jinsi alivyolazwa hospitali na Kassim alikwenda kumtazama siku za awali kabisa, kabla hata hawajaingia kwenye ulimwengu wa mapenzi.

Akakumbuka jinsi alivyolipia nusu ya matibabu yake, na Paulina pamoja na Pili walivyomwita jina la Baba Matokeo baada ya kukipita kitanda alichokuwa amelazwa.

Kwa wakati huo hata jina lake walikuwa hawalijui, bali ule tu utani wake wa kutoa jina hilo kwa mdoli wa Sauda, uliosababisha, Kassim kuitwa baba Matokeo, na Sauda naye kuwa mama Matokeo. Utani uliogeuka ukweli na kuanza kuwa wapenzi, baadaye ndoa.

"Basi Paulina sitokubali tena, nitapambana." Sauda akasema akionekana amefarijika.

**INAENDELEA JUMAPILI**

# NIKA, PANDA TZ WAMEKUJA KIVINGINE NA NGOMA MPYA



WASANII wa muziki wa kizazi kipya wanaokuja kwa kasi, Kamal Masala maarufu kama Mandh Tz na Nicole Piecha anayejulikana 'Nikanewmoon' wameachia ngoma yao mpya inayokwenda kwa jina la Kidogo IDK.

Akizungumza na Nipashe jana, Nicole amesema ameamua kumshirikisha Panda Tz kwenye wimbo huo ili kuchanganya ladha ya muziki wa Ujerumani ambako anakotoka na ule wa Bongo Fleva.

Amesema katika kibao hicho wamezungumzia kuhusu maisha, matatizo, matumaini na upendo wa Mungu kwa watu wote bila kujali taifa, dini na rangi.

"Ni wimbo unaelezea maisha ya kila siku yakiambatana matatizo, faraja na matumaini ya watu. Natumaini kila mtu ataupenda kutokana na ujumbe wake kulenga jamii yote," amesema Nikanewmoon,

Amesema wimbo huo ambao umetambulishwa jana katika majukwaa ya muziki upo katika mfumo wa Audio na kuanzia Februari video yake itakuwa tayari.

Kwa upande wa Pandah Tz, ambaye ni rapa kutoka Arusha amesema Watanzania watarajie kupata ladha ya kipekee kutoka kwenye mchanganyiko huo wa burudani.

"Watu wamezoea kuona wasanii wa aina moja wakishirikiana, lakini sisi tuko tofauti tumechanganya muziki hip hop ule wa Kijerumani ili kuwapa furaha,ameeleza Pandah Tz.

Aidha wasanii hao wawili wameeleza kuwa wanatarajia kufanya kazi nyingine siku zijazo na kuwaomba mashabiki wa muziki kuwaunga mkono katika wimbo wao mpya.



# Budju amaliza Utukufu Concert Uganda

STAA wa muziki wa Injili nchini Canada, Jonathan Budju, amemaliza kwa kishindo tamasha lake lililoitwa 'Utukufu Concert lililofanyika jijini Kampala.

Budju mwenye asili ya Congo ambaye anatamba na ngoma zake nyingi kama vile Tawala, Utukufu na Hosanna amekuwa nchini Uganda kwa muda wa mwezi mmoja akitumbuiza mashabiki zake na kutoa huduma mbalimbali za kiroho.

Pia kupitia taasisi yake ya Jonathan Budju Foundation, ametoa misaada mbalimbali kwa watu wasiojiweza.

Akizungumzia ziara hiyo, Jonathan amesema imekuwa na mafanikio makubwa na anafurahia kuona wamekuwa karibu na Mungu kupitia nyimbo zake.

"Nimesharudi nchini Canada lakini mawazo yangu bado yako Afrika, kwa sababu nimemuona Mungu akiwahudumia watu kwenye Utukufu Concert na mimi nimewagusa watoto waliopo kwenye mazingira magumu kupitia taasisi yangu," amesema Jonathan.

## ZISIKUPITE

### ONANA ATAKIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imemtambua kiungo wa kati wa Everton na Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 22, kama chaguo zuri la kuimarisha safu yao huku wasiwasi ukiongezeka kuhusu mustakabali wa kiungo wa kati wa Brazil, Joelinton mwenye umri wa miaka 27, ambaye bado hajakubali mkataba mpya katika uwanja wa St James' Park. (***Telegraph***)

### WEST HAM YATAKA WAWILI
KLABU ya West Ham inapania kufanya usajili wa mkopo mara mbili baada ya kuanzisha mazungumzo na Manchester City kuhusu mkataba wa kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, na kuwasiliana na Arsenal kuhusu Smith Rowe. (***Guardian***)

### GALLAGHER KUSITISHWA
KLABU ya Tottenham Hotspur itasitisha uhamisho wa kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, hadi msimu ujao baada ya mazungumzo juu ya mkataba wa Januari kuvunjika na sasa wanamuona Kalvin Phillips kama kiungo mbadala bora mwezi huu. ***(Football Insider)***

### ROWE HAUZWI
KLABU ya Arsenal imekataa mbinu za kumuuza Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 23, huku Aston Villa, West Ham na Newcastle zote zikionesha nia ya kumsajili kiungo huyo wa kati wa England ambaye amecheza mechi mbili tu katika mashindano yote msimu huu. ***(Mail)***

### WIRTZ AFUATILIWA
REAL Madrid, Bayern Munich na Manchester City zote zinamfuatilia kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa miaka 20, ambaye ana thamani ya zaidi ya pauni milioni 100. (***Bild***)

### BERGWIJN AWANIWA
MKURUGENZI wa masuala ya kifundi wa West Ham, Tim Steidten pia anaongoza juhudi za klabu hiyo kumsajili mshambuliaji wa Ajax, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 26 mwezi huu, licha ya kocha David Moyes kutoshawishika na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi. ***(Football Insider)***

### EDERSON AFUATILIWA
KLABU za Newcastle United na Liverpool zote zinamfuatilia kiungo wa kati wa Atalanta, Mbrazil Ederson mwenye umri wa miaka 24. ***(Gazzetta dello Sport)***

### BERGVALL AWINDWA
KLABU ya Manchester United inapanga kufanya mazungumzo na Djurgardens kuhusu uwezekano wa kumnunua kiungo, Lucas Bergvall mwenye umri wa miaka 17, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kung'ara katika soka barani Ulaya, akiwa tayari anachezea Sweden. (***90min***)

### LINGARD KUHAMIA MAREKANI
MCHEZAJI huru, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 31, yuko tayari kuhamia Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS. (***Mail***)

### DURAN MKATABA MFUPI
KLABU ya Chelsea inaweza kuvutiwa na mkataba wa mkopo wa muda mfupi kwa mshambuliaji wa Aston Villa, Colombia Jhon Duran mwenye umri wa miaka 20. (***Nathan Gissing, kupitia Metro***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MO SALAH KUKOSA MECHI MBILI AFCON

**Ni baada ya kuumia msuli wa paja kwenye mchezo dhidi ya Ghana uliomlazimu kutoka nje na kuepuka kupata.....**

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MOHAMED Salah anatazamiwa kukosa mechi mbili za Kombe la Mataifa ya Afrika baada ya kuumia msuli wa paja wakati Misri ikitoka sare na Ghana Alhamisi, lakini ameepuka majeraha makubwa zaidi, Shirikisho la soka la Misri limethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alichechemea mwishoni mwa kipindi cha kwanza cha sare ya 2-2 katika Kundi B, jambo lililozua hofu kwamba michuano yake ya AFCON imemalizika na wasiwasi kwamba ushiriki wake katika changamoto ya taji la Ligi Kuu ya Liverpool utathiriwa.

**Hata hivyo, taarifa ili yotolewa na EFA jana ilisema kwamba fowadi huyo anaweza kurejea uwanjani kwa ajili ya robo fainali ya AFCON Februari 2 na 3 kama Misri itafanikiwa kufika hatua hiyo.**

"Mohamed Salah amepata mkazo katika misuli yake ya paja na atakosa mechi mbili za Kombe la Mataifa ya Afrika," ilisema taarifa hiyo.

"Vipimo vya X-rays ambayo nahodha wa timu ya taifa ya Misri Salah alifanyiwa vilionesha kuwa alipata mkazo kwenye misuli ya nyuma, na atakosa mechi mbili zijazo za timu hiyo kwenye Afcon -- dhidi ya Cape Verde, na kisha mechi ya hatua ya 16 bora kama wakifuzu."

Misri watacheza na na wapinzani wao wa hatua ya makundi Januari 22 na wanaweza kufuzu kwa mechi ya hatua ya 16 bora, iliyopangwa kati ya Januari 27 na Januari 29.

Salah alikaa uwanjani kwa huzuni kwenye mechi ya Alhamisi, na aliondolewa mara moja baada ya kupokea matibabu uwanjani.

Jambo la kutia moyo ni kwamba nahodha huyo wa Misri aliweza kutembea hadi kwenye benchi -- ingawa kwa usumbufu fulani -- na baadaye alionekana akitabasamu alipokuwa akipitia eneo lenye mchanganyiko katika picha zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Akizungumza baada ya mechi, kocha mkuu Rui Vitória alielezea matumaini yake kwamba jeraha la Salah halikuwa kubwa, na sasa atakuwa na matumaini kwamba anaweza kurejea kucheza sehemu yake katika hatua za mwisho za shindano.

Akizungumza katika mkutano na wanahabari Ijumaa, kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp alifichua wasiwasi wake kuona Salah akibadilishwa kutokana na maumivu, akizingatia rekodi bora ya majeraha ya mshambuliaji huyo.

Iwapo Misri itatinga fainali ya Afcon, mechi ya kwanza ya Salah katika Ligi Kuu ya England inaweza kuwa ugenini huko Brentford mnamo Februari 17.

Huku Salah akiwa hayupo, Mohammed Kudus wa West Ham United aliifungia Black Stars mabao mawili kabla ya Omar Marmoush na Mostafa Mohamed wakisawazisha.

# MAKOSA YA ONANA YAISAIDIA SENEGAL KUFUZU 16 BORA



**YAMOUSSOUKRO,** Ivory Coast

ANDRE Onana alianza vibaya kampeni zake za Afcon baada ya kuruhusu mabao matatu dhidi ya mabingwa watetezi Senegal.

Ismaila Sarr alifunga bao moja na kutengeneza jingine huku mabingwa watetezi Senegal wakilaza Cameroon 3-1 Ijumaa na kujikatia tiketi ya kuingia hatua ya 16 bora katika Kombe la Mataifa ya Afrika, na kuwaacha wapinzani wao katika hatari ya kutolewa.

Sarr alifunga bao la kwanza katika kipindi cha kwanza cha mpambano huo wa Kundi C mjini Yamoussoukro baada ya makosa ya mlinda mlango wa Manchester United, Onana, ambaye alikuwa akicheza mchezo wake wa kwanza wa michuano hiyo baada ya kuchelewa kuwasili Ivory Coast.

Habib Diallo aliongeza bao la pili kutoka krosi ya Sarr kabla ya Jean-Charles Castelletto kuifungia Cameroon bao la kufutia machozi. Sadio Mane alifunga la tatu kwa a Senegal katika dakika za majeruhi.

Simba wa Teranga hao wametinga hatua ya mtoano wakiwa na mchezo wa mwisho wa makundi dhidi ya Guinea. Cameroon lazima icheze na Gambia katika mechi yao ya mwisho. Zote mbili ni Jumanne.

Senegal wanaongoza kundi wakiwa na pointi sita katika michezo yao miwili, wakati Cameroon na Guinea wana pointi moja na Gambia hawana.

Timu hizo mbili za mwisho zitakutana katika mchezo wa Ijumaa.

Cameroon ilimjaribu kwa shida kipa wa Senegal Édouard Mendy hadi dakika 10 za mwisho ambapo wangeweza kupata pointi, lakini umakini mdogo wa wachezaji wake ukawafanya washinde kupata mabao mengine.

# Kocha Gambia hajakata tamaa



**ABIDJAN,** Ivory Coast

KOCHA wa Gambia, Tom Saintfiet bado hajakata tamaa ya kufuzu hatua ya 16 bora kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika licha ya kufungwa 1-0 na Guinea Ijumaa katika Kundi C.

Akizungumza baada ya kupoteza, Saintfiet alikubali Guinea walikuwa bora katika kipindi cha kwanza kabla ya Gambia kuimarika baada ya mapumziko.

"Katika kipindi cha kwanza Guinea walikuwa na nguvu zaidi lakini kipindi cha pili tuliinua kiwango chetu zaidi," alisema raia huyo wa Ubelgiji.

"Nitabaki chanya kwa sababu tulifanya hivyo dhidi ya timu ngumu, yenye ubora kama Guinea."

Saintfiet alihisi Gambia iliunda nafasi za wazi na ilikuwa na bahati mbaya kwa bao lililokataliwa kabla ya ushindi wa Guinea.

"Bao dhidi yetu halikutarajiwa. Niliwashukuru wachezaji kwa sababu siwezi kuzungumza vibaya kuhusu timu ninayoongoza," aliongeza.

Licha ya kushindwa mara mbili, Saintfiet amesema bado wana nafasi akisema: "Bado tuko hai, hali imekuwa ngumu zaidi.

"Bado tunaweza kufuzu tukiwa na pointi tatu katika mchezo wetu ujao," alisisitiza.

Saintfiet alibainisha mabao ya kufunga kama ufunguo wa kuishinda Cameroon katika mechi yao ya mwisho ya kundi.

"Bado hatujafunga ili kushinda lazima tutafute mabao dhidi ya Cameroon," alisema.

# Camara: Kocha Diawara hututia moyo kila wakati

**ABIDJAN,** Ivory Coast

MFUNGAJI wa bao la Guinea, Aguibou Camara alisifu maneno ya kutia moyo ya kocha wao Kaba Diawara baada ya ushindi wao wa 1-0 wa Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Gambia.

Kiungo huyo wa kati wa Olympiacos mwenye umri wa miaka 22 alifunga bao pekee Ijumaa na kutangazwa mchezaji bora wa mechi hiyo.

"Ninakabidhi tuzo hii kwa marehemu baba yangu," alisema Camara baada ya mechi. "Nitaendelea kucheza kwa bidii, niko katika kiwango hiki kutokana na msaada wa familia yangu."

Camara pia alisema mchango wa Diawara kwenye kikosi wakati wa michezo.

"Kaba ni kocha anayetusukuma kucheza kwa bidii, kwenye chumba cha kubadilishia nguo anazungumza na sii na kututia moyo sana wakati wa mechi," alieleza Camara.

Mfungaji huyo alisisitiza kuwa ana furaha kucheza popote inapohitajika kwa timu.

"Mimi ni mchezaji lazima niendelee kuwepo kwenye timu. Ninapocheza nje, lazima nifanye vizuri," alisema Camara.

"Sio mimi ninayechagua nafasi yangu, ninajiweka tayari kusaidia timu ya Guinea."

Baada ya mechi nzuri ambapo aling'ara katika nafasi ya kiungo ya juu, Camara alifichua msukumo nyuma ya onyesho lake.

Mazungumzo ya timu ya Diawara yaligusa gumzo wazi huku Guinea ikidai ushindi muhimu dhidi ya Gambia.

Nyota huyo mchanga anatumaini kuwa na matokeo zaidi katika mpambano mkubwa wa Kundi C Jumanne dhidi ya mabingwa watetezi Senegal.



HABARI MICHEZO

# GAMONDI KUSAKA MAKALI KWA JKU

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi aliagiza uongozi wa timu hiyo kumtafutia michezo angalau miwili ya kirafiki kwa ajili ya kukipima kikosi chake, na sasa timu hiyo itaanza kujipima na JKU ya Zanzibar kabla ya kurejea katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo huo wa kwanza wa kirafiki utachezwa Jumamosi ijayo kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.

Viongozi wa Yanga wamelazimika kusaka mechi za kirafiki mapema baada ya Gamondi kuwaambia wafanye kila linalowezekana kupata mechi za haraka kabla ya kurejea kwa Ligi Kuu.

Hata hivyo, kutoka ndani ya klabu hizo zinasema wamekubaliana kuhusu kucheza mechi hiyo ya kirafiki na JKU na wapo kwenye mchakato wa kusaka timu nyingine ya pili kukamilisha hitaji la kocha Gamondi.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi alisema kuna kila sababu ya timu yake kupata mechi za kirafiki, ikiwezekana pia na mchezo mmoja wa kimataifa wa kirafiki wakati huu wa mapumziko ili kujua ubora wa kikosi chake na kuona muunganiko alioutengeneza.

"Tumerejea mapema kwenye mazoezi kuweza kujipanga kwa muda huu ambao upo kwa sasa, unajua tuna wachezaji wapya ambao wamesajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo la usajili, tupo nao kwenye mazoezi hivyo ni vizuri kupata michezo ya kirafiki kuangalia kikosi chetu," alisema Gamondi na kuongeza,

"Tunalenga kuboresha timu yetu tukiwa na malengo ya kufanya vizuri kimataifa, michezo hii ya kirafiki baada ya kuongeza wachezaji itanipa picha ya nini napaswan kuongeza au kuboresha," alisema Gamondi.



## Morocco: Stars tutaingia kwa tahadhari leo

INATOKA UK. 24


Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo alisema kwa yote yaliyotokea ni lazima timu iendelee na mashindano, hivyo kuwataka mashabiki wa soka na Watanzania wote wawe pamoja na timu yao.

"Vyovyote itakavyokuwa timu lazima iendelee, bado tuko kwenye mashindano, lazima kuwe na walimu mbadala, hali ya kambi ipo vizuri wachezaji wapo kwenye morali na ari kubwa kuelekea kwenye mchezo wetu dhidi ya Zambia, ni kweli tumepoteza mchezo wa kwanza dhidi ya Morocco lakini haina maana kuwa tumepoteza mashindano, bado nafasi tunayo kwa jinsi kundi letu lilivyokaa, nia yetu ya dhati ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi zetu mbili zinazofuata ili tusonge mbele," alisema Ndimbo.



Wakati Stars ikienda kucheza dhidi ya Zambia itakuwa imeshapata matokeo ya kundi lake kati ya Morocco dhidi ya DR Congo ambao watatangulia kucheza saa 11:00 jioni.

Zambia ina pointi moja iliyoipata baada sare ya 1-1 dhidi ya DR Congo, Stars ikiwa haina pointi ambapo ni ushindi tu unaoweza kuifanya kuendelea kuwepo kwenye mashindano hayo na matokeo mengine tofauti na hayo itakuwa imejiweka kwenye wakati mgumu zaidi.




Mshindi wa magifti dabodabo, Mohamed Salum (kulia) akipokea mfano wa hundi ya shilingi milioni moja kutoka kwa Meneja wa Wateja Maalum wa kampuni ya Tigo, Mary Rutta baada ya droo ya wiki ya nane ya promosheni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wazawa hawashikiki ufungaji Ligi Kuu Wanawake

**Na Oliver Albert**

VITA ya ufungaji bora imeendelea kuwa kubwa kwenye Ligi Kuu ya wanawake Tanzania Bara msimu huu huku wazawa wakionekana kuwa wa moto zaidi. Kwa misimu miwili mfululizo tuzo ya ufungaji bora ilienda kwa wachezaji wa kigeni ambapo msimu uliopita akichukua Mkenya, Jetrix Shikangwa baada ya kufunga mabao 17 na msimu wa 2021/2022 mrundi Asha Djafar alitwaa tuzo ya ufungaji bora kwa kufunga mabao 27.

Msimu huu ni kama wazawa wameona imetosha sasa ni zamu yao kurudisha ufalme wao kwani wamekuwa wakifunga kila mara katika ligi hiyo inayoendelea nchini.

Mara ya mwisho mzawa kutwaa tuzo ya ufungaji bora ilikuwa msimu wa 2020/2021 baada ya aliyekuwa mchezaji wa Yanga Princess , Aisha Masaka kumaliza kinara kwa kufunga mabao 35 mbele ya Opah Clement aliyekuwa Simba Queens aliyefunga mabao 34.

Wachezaji hao wote wawili kwa sasa wanacheza soka la kulipwa nje ya nchi, Aisha akicheza katika klabu ya BK Hacken ya Sweden wakati Opah anaichezea Beskitas ya Uturuki.

Msimu huu Aisha Mnuka wa Simba Queens ndiye kinara akiongoza orodha yaufungaji bora baada ya kufunga mabao nane akifuatiwa na Winfrida Gerald na Stumai Athuman' Kuchi' wote wa JKT waliofunga mabao sita kila mmoja.

Msimu uliopita Aisha hakuwa akipata nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Simba na alimaliza na bao moja tu wakati Winfrida ambaye alikuwa akiichezea Founta Gate alimaliza na mabao tisa huku Stumai akimaliza na mabao 13.

Kocha wa Alliance Girls, Ezekiel Chobanka alisema anaona msimu huu ni kama wazawa wameamua kurudisha heshima yao.

"Wazawa wameanza na moto sana na wako katika kiwango bora kama wataendelea hivi basi msimu huu unaweza kuwa mzuri kwao na tuzo ya ufungaji wakachukua, "alisema Chobanka.

## *Wanachama Simba kuamua hatma ya Katiba yao leo*

INATOKA UK. 24

wazi kwenye katiba, nne ni Mkutano Mkuu wa namna ya kupata akidi ya wanachama watakaoweza kufanya mkutano ufanyike, kuangalia haja ya kuwa na chombo cha Simba Sports Club Limited kitakachoshikiri hisa za Simba au la na jambo la sita ni hili suala la ndani ya kampuni kuna asilimia 99 zinazoshikiliwa na bodi ya wadhamini moja inashikiliwa na Mwenyekiti, sasa Serikali inataka katiba iseme kuwa hiyo si yake, hawezi kuiuza, kuihamisha na kwamba anaishikilia kama mdhamini ili kuilinda ambapo isitokee siku moja kuamua kuiuza. Vikifanyiwa kazi hivi, basi moja kwa moja serikali itabariki mabadiliko ya uendeshaji wa kisasa wa klabu jambo ambalo wanachama na mashabiki wengi wa Simba wanalisubiri," alisema Kitta.

Mchakato wa Mabadiliko ya Klabu ya Simba ulioanza tangu 2017, na umekuwa haukamiliki kwa asilimia 100 kutokana na matatizo mbalimbali ya ndani na nje ya klabu hiyo.

# Michezo

Jumapili Januari 21, 2024

Nipashe


UKU. 22



**Makosa ya Onana yaisaidia Senegal**



Kaimu Kocha Mkuu wa timu ya taifa 'Taifa Stars', Hemed Moroco (katikati) akizungumza na Nahodha wa timu hiyo Mbwana Samatta (kushoto) na msaidizi wake, Himidi Mao baada ya mazoezi ya timu hiyo juzi kuelekea kwenye mchezo wa leo dhidi ya Zambia. **PICHA: MTANDAO**

# *Wanachama Simba kuamua hatma ya Katiba yao leo*

## ●●● Ni katika mkutano Mkuu utakaotoa jibu la mabadiliko ya uendeshaji ndani ya....

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WANACHAMA wa klabu ya Simba leo wanatarajia kufanya maamuzi magumu ya kukataa au kupitisha marekebisho ya Katiba ya Klabu hiyo kongwe kama ilivyopendekezwa na Serikali.

Wanachama hao watapata fursa leo kwenye Mkutano utakaofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere, Posta jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa kamati ya Katiba na Sheria wa klabu hiyo, Hussein Kitta, amesema kila kitu kimekwenda vizuri na kilichobaki ni wanachama wenyewe kuamua kuipitisha au la.

"Wanachama waje, wasikilize, lakini pia wapate fursa ya kuamua, wakipitisha ni katiba yao, wakikataa simba ni ya kwao, lakini wakumbuke hii inafanywa kwa ajili ya kuitoa Simba hapa na kuipeleka hatua nyingine," alisema Kitta.

Kwa mujibu wa Kitta, Serikali iliwaita na kuwaambia baadhi ya vifungu haviendani na sheria ya nchi, hivyo wakavirekebishe kwa ajili ya kurahisisha mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji uweze kukamilika.

"Waziri mwenye dhamana ya michezo, Dk. Damas Ndumbaro, aliitisha kikao kujadili kuhusu mchakato wa mabadiliko wa Simba na kukawa na mambo sita ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi. Kutokana na mkutano huo bodi ya Simba ikaunda kamati hii. Tulipokea maoni mengi, mengine kwa barua pepe, mengine kwa barua za kawaida, wengine kutupigia simu na kututumia ujumbe, tulikaa vikao vinne kwa kati ya saa sita mpaka tisa kupitia," alisema Kitta na kuongeza.

"Mchakato wa maboresho ya katiba umefanyika ili kutekeleza maagizo ya Serikali yaliyotaka mabadiliko kwenye maeneo mahususi ili kukidhi matakwa ya kisheria, hivyo basi, lengo ni kukamilisha mabadiliko na Serikali ilitupa muda ili kukamilisha jambo hili, BMT (Baraza la Michezo la Taifa) walisema kabla ya kupeleka kwa wanachama tuwapelekee rasimu kwanza. Baada ya vikao tukaenda BMT na tukapokea barua ya kuridhishwa na yale tuliyopitisha," alisema Kitta.

Alisema baadhi ya vifungu vilivyorekebishwa na vinavyotarajiwa kupitishwa au kutopitishwa ni mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa bodi, kwa katiba ya sasa wanateuliwa na bodi ya wakurugenzi.

"Na sasa mapendekezo yanataka wateuliwe na Mkutano Mkuu wa Wanachama, nafasi ya Mwenyekiti wa Klabu ya Simba iwe wazi jinsi anavyopatikana kwa kuwa katika katiba ya sasa haiko wazi, tatu ni malengo ya klabu yanatakiwa yaelezwe

INAENDELEA UK. 23

# Morocco: Stars tutaingia kwa tahadhari leo

**Na Adam Fungamwango**

KAIMU Kocha Mkuu wa timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Hemed Morocco amesema wataaingia kwa tahadhari kubwa katika mechi ya leo dhidi ya Zambia kwa sababu ni muhimu kwenye mustakabali wa ushiriki wa fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazoendelea nchini Ivory Coast.

Stars inashuka kwenye Uwanja wa San Pedro, saa 2:00 usiku kucheza dhidi ya timu jirani, ikiwa ni mechi ya raundi ya pili ya fainali hizo kwenye Kundi F.

Hata hivyo Stars itacheza mechi hiyo bila ya kocha wake Adel Amrouche ambaye amefungiwa mechi nane na Kamati ya Nidhamu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kwa kile kinachodaiwa kuongea maneno ya uchochezi dhidi ya shirikisho hilo.

Hatua hiyo ililifanya pia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kumsimamisha kwa muda usiojulikana kocha huyo raia wa Algeria.

"Haitokuwa mechi rahisi kwa sababu Zambia ni timu nzuri, tutaingia kwa tahadhari kwani nao wanahitaji ushindi kwa kuwa mechi iliyopita walitoka sare na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, huwezi kujua nao watatoka vipi na Morocco kwa hiyo utaona kundi ni gumu na kila mmoja anataka matokeo mazuri, lakini tumefanya mazoezi mazuri ya kutosha na tumerekebisha makosa ya mechi ya kwanza, naamini tutafanya vizuri," alisema Morocco ambaye kwa sasa atasaidiana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Coastal Union miaka ya 1980, Juma Mgunda kama kocha msaidizi.

Morocco alisema ushindi kwenye mchezo wa leo ni muhimu kwa sababu utairudisha timu kwenye mstari wa kuendelea kupigania kusonga mbele na kutinga hatua ya robo fainali.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >